# Nipashe

Ijumaa Aprili 9, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580545

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



Samia chungulia matobo zaidi uyazibe

Ile UTT, mfuko unaosajili tafsiri kuu ya uchumi binafsi na uwekezaji kimkakati

BUFE

Corona inavyowadororesha wafanyabiashara wa bidhaa kutoka ukanda wa ughaibuni

IJUMAA APRILI 9, 2021 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Wakulima korosho, ushirika wao Liwale wajipanga baada kombora

- Mrajisi Ushirika: Ndio kilimo kilivyo!
- Mwenyekiti Ushirika aanika mikakati

UKURASA 11

**Watumiaji** wa Stendi ya Magufuli waeleza kero

UKURASA 4



**Mtalaam** wa afya aeleza athari kwa wagonjwa wa corona

UKURASA 9

# Madudu mazito ripoti ya CAG

- **Upigaji** wa kutisha Utalii, akaunti Zimamoto yapitisha malipo batili, bil. 3.92/- zatengeneza ndege...*Ukurasa 2,3,8,9*



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, akiwasilisha ripoti kuu ya mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2020 jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Waziri aingia matatani bungeni

UKURASA 4



## Spika aagiza mjadala hasara mabilioni ATCL

UKURASA 4

**MICHEZO** **SIMBA, AL AHLY KAZI IENDELEE** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Bil. 5.14/- ushuru forodha hazikuthibitishwa

**Na Romana Mallya**

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), imebainisha matatizo ya ukusanyaji wa mapato kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ikiwamo bidhaa zilizopita kwenda nchi jirani zenye ushuru wa forodha wa Sh. bilioni 5.14, hazikuthibitishwa kutoka nchini.

Katika ripoti hiyo ya CAG Charles Kichere, aliyoisoma jana bungeni jijini Dodoma, alisema TRA ilikuwa na changamoto mbalimbali katika ukusanyaji mapato.

"Katika ukaguzi wangu wa bidhaa zinazopita nchini kuelekea nchi jirani kupitia mipaka ya forodha ya Tunduma, Kasumulu, Rusumo, Kabanga, Mutukula, Namanga, Holili na Kigoma kwa kuangalia mfumo wa TANCIS na nyaraka za kusafirishia sikuthibitisha kuwa bidhaa zenye makadirio ya kodi ya forodha ya Sh. bilioni 5.14 zilitoka nchini," alisema.

Ripoti hiyo pia imeeleza mafuta yaliyopitiliza muda nchini ambayo yalipaswa kwenda nchi jirani yenye ushuru wa forodha Sh. bilioni 12.14, yalibainika lita milioni 2.47 zenye makadirio ya ushuru wa forodha wa Sh. bilioni 1.97 yalibaki Tanzania bila kusafirishwa kwenda nchi zilizokusudiwa kwa muda uliopangwa wa siku 30.

Pia, lita milioni 14.08 za mafuta zenye ushuru wa forodha unaokadiriwa kufikia Sh. bilioni 10.43 zilizoshushwa ili kusafirishwa kwenda Zanzibar tangu mwezi Julai, 2019 hazijaondoshwa kwa muda uliopangwa wa siku 21.

"Kwa mujibu wa sheria ya forodha, mafuta yanayokaa nchini kwa zaidi ya muda uliopangwa yanapaswa kurasimishwa kwa matumizi ya ndani na hivyo kutozwa ushuru unaotakiwa," alisema.

CAG katika ripoti hiyo alibainisha kodi zilizoshikiliwa na kesi zilizopo katika mamlaka za rufaa za kodi ni Sh. trilioni 360 na Dola za Marekani milioni 181.

"Nimebaini kuwa TRA imekuwa na kesi 1,097 za muda mrefu katika Mamlaka za Rufaa za Kodi zenye thamani ya Sh. trilioni 360 na Dola za Kimarekani milioni 181," alisema.

Kadhalika, mwaka 2019/20, TRA ilikusanya Sh. trilioni 17.92 dhidi ya makisio yaliyowekwa ya Sh. trilioni 19.41, na kuwa na upungufu wa makusanyo kwa Sh. trilioni 1.49 sawa na asilimia nane ya jumla ya makisio ya makusanyo.

**DENI LA SERIKALI**

Deni la serikali hadi kufikia Juni 30, mwaka jana, lilikuwa Sh. trilioni 56.76 na la ndani lilikuwa Sh. trilioni 15.52, la nje Sh. trilioni 41.24, ikiwa ni ongezeko la Sh. trilioni 3.65 sawa na asilimia saba ikilinganishwa na deni la Sh. trilioni 53.11, liliporipotiwa mwaka wa fedha 2018/19.

Ongezeko hilo linajumuisha Sh. bilioni 652 za deni la ndani na Sh. trilioni tatu za deni la nje.

"Hadi Juni 30, mwaka 2020 deni la serikali lilikuwa linahimilika," alisema.



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, akiwasilisha ripoti kuu ya mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2020 jijini Dodoma jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Grace Tendega na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Japhet Hasunga. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CAG abaini madudu Wizara

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amebaini dosari nyingi katika Wizara ya Maliasili na Utalii ukiwamo ulaji wa mamilioni ya shilingi.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/20 iliyowasilishwa bungeni jijini Dodoma jana, CAG alisema amebaini usimamizi usioridhisha wa fedha za Mfuko wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii Sh. bilioni 34.985.

Alisema kuwa alibaini Sh. bilioni 6.875 zililipwa kutoka kwenye mfuko bila ya idhini ya Ofisa Masuuli kinyume cha Kanuni za Fedha.

Pamoja na hayo, CAG pia alibaini matumizi ya jumla ya Sh. bilioni 16.363 bila ya kuwa na hati za malipo na matumizi mengine ya jumla ya Sh. bilioni 11.157 ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi.

"Sh. milioni 89 zilitumiwa na Makumbusho ya Taifa, matumizi yasiyoendana na shughuli za utalii. Pia, ukaguzi wangu ulibaini kuwa kiasi cha Sh. milioni 500 kililipwa na Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA) moja kwa moja kwa Bodi ya Utalii ya Taifa bila kupitia kwenye akaunti ya Tozo za Maendeleo ya Utalii.

"Hii ni kinyume cha Kanuni ya 9(1) na (2) ya Kanuni za Tozo za Maendeleo ya Utalii za Mwaka 2013. Pia, nilibaini kuwa hadi kipindi cha ukaguzi, Kamati ya Ushauri ya Mfuko haikuwa imeundwa, kinyume cha Kanuni Na. 9(3) na 9 (4) (a-g) ya Kanuni za Tozo za Maendeleo ya Utalii za Mwaka 2013.

"Mapungufu hayo yanaonyesha kuwa akaunti ya tozo hizo haikusimamiwa ipasavyo na Mkurugenzi wa Utalii na mhasibu ambapo walitoa fedha bila ya idhini ya Kamati ya Ushauri na Ofisa Masuuli wa Wizara kufahamishwa.

"Kwa maoni yangu, Mkurugenzi wa Utalii na Mhasibu waliokuwa wanahusika na usimamizi wa Mfuko wa Makusanyo ya Tozo za Maendeleo ya Utalii, walitumia vibaya fedha za tozo za utalii jumla ya Sh. bilioni 34.98 kinyume cha Kanuni ya Tozo za Maendeleo ya Utalii za Mwaka 2013," alisema.

**TAMASHA LA URITHI**

CAG alisema ukaguzi wake kuhusu Tamasha la Urithi ili kukuza utalii na urithi wa kitaifa, alibaini kamati iliyoundwa iliidhinisha bajeti ya Sh. bil 1.6 kwa ajili ya utekelezaji wa hafla hiyo.

Hata hivyo, alisema bajeti hiyo haikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na hakukuwa na mpango wa utekelezaji wa Tamasha la Urithi.

Kutokana na kukosekana kwa mpango wa utekelezaji ulioidhinishwa, CAG alibaini Wizara ya Maliasili na Utalii iliomba wakala wake wanne kuchangia jumla ya Sh. bilioni moja ambazo hazikuwa kwenye bajeti zao ili kuwezesha kufanyika kwa tamasha hilo.

"Ili kuongezea bajeti hiyo, Wizara ya Maliasili na Utalii ilichangia Sh. milioni 299 na Mfuko wa Tozo wa Maendeleo ya Utalii ulichangia Sh. milioni 270.84; jumla ya Sh. bilioni 1.57 zilipatikana ili kufanikisha utekelezaji wa tamasha hilo ambapo fedha zote hizi hazikuwa kwenye bajeti za wizara na taasisi husika.

"Wakati wa utekelezaji, nilibaini kuwa Kituo cha Televisheni cha Clouds na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) walilipwa jumla ya Sh. milioni 629.7 na Sh. milioni 201.46, Mtawalia, kwa ajili ya kuonyesha matangazo ya Tamasha la Urithi.

"Hata hivyo, hakukuwa na risiti za kielektroniki zilizotolewa kuthibitisha kupokelewa kwa malipo hayo. Aidha, kodi ya zuio ya Sh. milioni 31.49 na Sh. milioni 10.07 kutoka Kituo cha Televisheni cha Clouds na TBC haikukatwa katika malipo yaliyofanyika.

"Vilevile, sikupewa ushahidi unaoonyesha kuwa ununuzi wa huduma za matangazo kutoka TBC na Kituo cha Televisheni cha Clouds zilipatikana kwa njia ya ushindani na usawa," alisema.

CAG alisema alibaini jumla ya Sh. milioni 487.26 zilipelekwa kwenye taasisi saba kwa ajili ya utekelezaji wa Tamasha la Urithi.

Hata hivyo, hakukuwa na nyaraka zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ili kuthibitisha matumizi hayo na alibaini matumizi ya Sh. milioni 585.52 yaliyolipwa na Mhasibu wa Mfuko wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii bila ya kuwa na nyaraka toshelezi.

"Nilibaini kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ililipa Sh. milioni 140 kwa Kampuni ya Wasafi kwa ajili ya wasanii ambao wangetangaza utalii wa ndani katika mikoa sita ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Moshi, Iringa na Dodoma.

"Hata hivyo, hakukuwa na mkataba wowote uliosainiwa kati ya Kampuni ya Wasafi na Wizara ya Maliasili na Utalii. Hivyo, sikuweza kuhakiki wigo wa kazi pamoja na huduma zilizotolewa na kampuni ya Wasafi.

"Pia, kulikuwa na maagizo ya Waziri wa Maliasili na Utalii yakielekeza malipo kwa Kampuni ya Wasafi. Katika mahojiano na Waziri huyo, alikiri kuwa Kampuni ya Wasafi iliomba zabuni ya kutangaza tamasha hilo kwenye mikoa iliyotajwa na kutoa maagizo ya kufanya malipo hayo.

"Ni maoni yangu kuwa kiasi cha Sh. milioni 140 kilicholipwa kwa kampuni ya Wasafi kufuatia maelekezo ya Waziri wa Maliasili

HABARI KITAIFA



# ya Utalii

na Utalii, hakiendani na Sheria za Matumizi ya Fedha za Umma.

"Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro (NCAA) zilifadhili Tamasha la Upandaji wa Mlima Kilimanjaro bila ya kuwapo kwenye bajeti - Sh. 171,998,045.

"Mnamo tarehe 28 Septemba 2019, Waziri wa Maliasili na Utalii alizindua shindano liliitwa Kigwangalla Kili Challenge la mwaka 2019 lililolenga kuhamasisha watu kupanda Mlima Kilimanjaro. Shindano hilo lilitumia jumla ya Sh. milioni 172 zilizotolewa na NCAA (Sh. Milioni 114.5) na TANAPA (Sh. Milioni 57.5) bila kuwa katika bajeti zao za mwaka wa Fedha 2019/20.

"Pia, nilibaini kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kupitia kaimu katibu wake, alizielekeza NCAA na TANAPA kufadhili shindano hilo.NMT (Sh. 115,020,000), Arusha (Sh. 130,000,000), Dodoma (Sh. 24,338,000), Dar es Salaam (Sh.77,900,000), Mwanza (Sh. 60,000,000), Arusha (Sh. 30,000,000) na BASAZA (Sh. 50,000,000).

"Fedha iliyotolewa na TANAPA ililipwa kwa Kampuni ya Utalii ya Ahsante Tours and Safaris Sh. 57,498,045 kwa ajili ya gharama za malazi za wapandaji mlima.

"Nilibaini kuwa, Kaimu Katibu wa Waziri wa Maliasili na Utalii alitoa maagizo kwa NCAA na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kulipia matumizi ya Ofisi ya Waziri Sh. milioni 92.3 na Sh. milioni 55.93 kwa niaba ya Wizara ya Maliasili na Utalii, mtawalia.

"Taasisi hizo hazikuwa na bajeti ya malipo hayo; na ukaguzi wangu ulibaini baadhi ya shughuli za taasisi zilizowekwa katika mipango yao hazikutekelezwa," alisema.

# Akaunti Zimamoto yapitisha malipo batili

**Na Mwandishi Wetu**

RIPOTI ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Fedha za Serikali (CAG), imebaini akaunti ya masurufu ya Jeshi la Zimamoto ilitumika kupitishia malipo batili ya Sh. milioni 261.3

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali (CAG), Charles Kichere, alisema ofisi yake ilibaini kuwa kiasi hicho kiliwekwa katika moja ya benki za biashara kwa vipindi tofauti.

Kichere alisema Menejimenti ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji haikutambua vyanzo vya fedha hizo na hakukuwa na mawasiliano yoyote yaliyofanywa na benki kuhusu mapokezi ya fedha hizo.

Pia alisema alibaini kuwa fedha hizo zilichukuliwa na mtunza fedha wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutoka katika akaunti hiyo kwa vipindi tofauti kwa kutumia nyaraka za fedha za kughushi.

CAG alisema alibaini usuluhishi wa taarifa za benki kwenye akaunti ya masurufu haukufanywa kwa kipindi cha kuanzia Julai Mosi, 2019 hadi tarehe ya kukamilisha ukaguzi.

"Hii ni kinyume cha Kanuni Na. 162 (1) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 ambayo inahitaji taarifa za fedha za benki zifanyiwe usuluhisho angalau kila mwezi," alisema Kichere.

Alisema hali hiyo inaashiria kuwapo kwa udhibiti dhaifu wa mifumo ya ndani kwenye usimamizi wa fedha katika akaunti za benki za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

# Bil. 3.92/- zatengeneza ndege mbovu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Ndege za Serikali (TGFA), imelipa Sh. bilioni 3.92 kwa ajili ya matengenezo makubwa ya ndege aina ya Fokker 28-5H-CCM ya mwaka 1978.

Taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imebainisha kuwa malipo hayo yalifanyika kati ya Februari 14 na Aprili 24, 2018.

Hata hivyo, katika taarifa hiyo alisema wakati wa ziara yake kwenye hifadhi ya ndege za serikali, Dar es Salaam Agosti 19, 2020, alibaini kuwa ndege hiyo ilikuwa haifanyi kazi na ilikuwa imetelekezwa tangu mwaka 2015. Aidha, CAG alisema aligundua kuwa, TGFA iliwasilisha suala hilo Wizara ya Fedha na Mipango ikiomba ifanyike tathmini ya kina kuhusu ndege hiyo ili kuishauri serikali juu ya uamuzi sahihi wa hatua za kuchukua.

"Hata hivyo naona uamuzi wa kuwekeza fedha za walipa kodi zenye thamani ya Sh. bilioni 3.92 kufanya ukarabati mkubwa wa ndege bila kufanya tathmini ya kina ya gharama na faida haukuwa sahihi na hivyo, kusababisha hasara kwa taifa," alisema.

**MADUDU TEMESA**

CAG Kichere alisema makusanyo ya kivuko ambayo hayajapelekwa benki na hayapo kituoni ni Sh. 81,194,650. Alisema alibaini kuwa Kituo cha Kivuko cha Magogoni kilikusanya Sh. bilioni 5,757,041,950 ikiwa ni tozo za kivuko kwa kipindi kilichoanzia Julai, Mosi, 2019 hadi Juni 30, 2020.

Hata hivyo, kati ya pesa zilizokusanywa ni Sh. 5,675,847,300 ndizo zilizowekwa kwenye akaunti ya benki inayosimamiwa na Makao Makuu ya TEMESA, ikiacha jumla ya kiasi cha Sh. 81,194,650 kikiwa bado hakijawekwa benki hadi muda wa ukaguzi, tarehe 31 Julai 2020.

Aidha, alisema kuwa alibaini kuwa kiasi hicho cha fedha ambacho hakikuwekwa benki pia hakikuwa kwenye himaya ya kituo.

"Kwa maoni yangu fedha hizi ambazo hazijawekwa benki kuna uwezekano kwamba zimetumiwa vibaya au kutumiwa katika shughuli zingine," alisema.

Alisema alibaini kuwa TEMESA iliuza jumla ya tiketi 21,447,004 zenye thamani ya Sh. bilioni 5.76 lakini ni tiketi 9,122,690 tu zenye thamani ya Sh. bilioni 3.16 ndizo zilizothibitishwa na mashine na kuacha tiketi 12,324,314, zenye thamani ya Sh. bilioni 2.60 zikitumika bila ya kuthibitishwa na mashine.

"Ni maoni yangu kuwa, tiketi hizo zinaweza kutumika tena na kusababisha serikali kupoteza mapato," alisema Kichere.

# Mapingamizi kodi za bil. 38.8/- yacheleweshwa

**Na Romana Mallya**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amesema katika ukaguzi wake Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), amebaini uwapo wa mapingamizi 44 yenye kodi ya thamani ya Sh. Bilioni 38.8.

Hayo yamo kwenye ripoti yake aliyoisoma jana bungeni jijini Dodoma huku akibainisha ucheleweshaji huo wa utatuzi wa mapingamizi hayo. "Nilibaini uwapo wa mapingamizi 44 yenye kodi ya thamani ya Sh. Bilioni 38.78 katika idara ya walipakodi wakubwa, idara ya upelelezi wa kodi na idara ya kodi za ndani ambazo hayajatatuliwa kwa muda uliotakiwa kama ilivyoainishwa katika mkataba wa huduma na mlipa kodi ya mwaka 2017," alisema.

Kichere alisema kucheleweshwa kwa utatuzi wa mapingamizi ya kodi kunaathiri malengo ya ukusanyaji wa kodi kwani mapingamizi hayo yanafunga kiasi kikubwa cha kodi," alisema.

Alisema amebaini kutokusanywa kwa ushuru wa forodha kwa magari na bidhaa (mitambo) zilizoingizwa nchini kwa muda ambazo hazijaondolewa baada ya muda kuisha

"Nilibaini magari 936 yaliyoingizwa nchini kwa muda kupitia mipaka ya forodha ya Namanga, Holili, Tarakea, Mtambaswala na Sirari yamebaki nchini kwa zaidi ya muda ulioruhusiwa bila uthibitisho wa maombi ya waingizaji kuongezewa muda," alisema.

Pia alisema alibaini bidhaa (mitambo) zenye thamani ya Sh. Bilioni 20.25 na ushuru wa forodha Sh. Bilioni 1.24 zilizoingizwa kwa muda nchini kupitia mipaka ya Namanga, KIA, Holili na Bandari kavu hazijaondolewa.

Alisema hazijaondolewa baada ya kumalizika kwa muda ulioruhusiwa kuwapo Tanzania, wala hazijarasimishwa kwa matumizi ya ndani kama sheria ya forodha inavyoelekeza.

# Wizara zakopa bil. 4/- bila kurejesha

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA mbalimbali za serikali zimekopa Sh. bilioni 4.083 kutoka mifuko maalumu mitatu bila ya kurejesha fedha hizo.

Hiyo imo katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini Dodoma jana.

Alisema ni maoni yake kuwa kutokurudishwa kwa fedha zilizokopwa na wizara kunaathiri utekelezaji wa shughuli za mifuko maalumu, hivyo fedha hizo zirejeshwe ili kutekeleza shughuli zilizopangiwa.

Alisema katika ukaguzi wa mwaka huu, amebaini malipo yenye thamani ya Sh. bilioni 13.061 ambayo hayakuwa na nyaraka za kujitosheleza kinyume na Kanuni 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma 2001.

Alisema ni maoni yake kuwa chanzo cha kuwa na matumizi yenye nyaraka pungufu ni kuwa na mfumo dhaifu wa udhibiti na maofisa masuuli kushindwa kuchukua hatua stahiki kwa maofisa wanaosababisha udhaifu huo.

"Ninaamini kuwa hii inaweza kuwa ishara ya kufanyika kwa matumizi ya udanganyifu na mabaya. Mawanda yangu ya ukaguzi yalizuiwa hivyo sikuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika," alisema.

CAG alisema katika ukaguzi wa mwaka huu, alifanya ukaguzi wa usimamizi wa bajeti kwa taasisi mbalimbali na kubaini kuna malipo yenye thamani ya Sh. bilioni 29.6 yaliyofanywa nje ya bajeti kinyume na Kanuni ya Fedha za Umma ya 2001.

Alisema Kifungu Namba 49(3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka, 2011 kinaangiza Taasisi za ununuzi kuzingatia mpango wa ununuzi wa Mwaka.

Hata hivyo, CAG alisema katika ukaguzi wa Wizara, Idara, na Sekretarieti za Mikoa, taasisi saba zilibainika kufanya ununuzi wa vifaa na huduma wenye thamani ya Sh. bilioni 15.1 nje ya mpango wa mwaka wa ununuzi.

Alisema ikilinganishwa na mwaka 2018/2019, kuna ongezeko la Sh. bilioni 11.5 kwa ununuzi uliofanyika bila ya kufuata Mpango wa Ununuzi wa Mwaka.

Katika mwaka wa 2018/19, CAG alisema jumla ya taasisi saba zilifanya ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh bilioni 3.6 nje ya Mpango wa Ununuzi wa Mwaka.

"Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa Wizara mbili zilifanya matumizi kiasi cha Sh. Milioni 453.7 ambayo hayana tija.

# Watumiaji stendi ya Magufuli walia kero

**Na Elizabeth Zaya**

WATUMIAJI wa stendi ya Magufuli mkoani Dar es Salaam inayotumiwa na mabasi ya kusafirisha abiria waendao mikoani na nchi jirani, wamesema kero wanazozipata katika stendi hiyo ni kubwa tofauti na walivyokuwa wakitegemea.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, watumiaji hao wakiwamo baadhi ya wafanyabiashara wadogo na abiria, wamesema badala ya kituo hicho kuwa msaada kimekuwa ni kero.

Miongoni mwa mambo wanayolalamikia ni pamoja na kuzuiwa kwa mabasi ambayo ofisi zao ziko nje ya stendi hiyo kutokutoka au kuingia na abiria ndani ya stendi hiyo.

"Yaani stendi imewekwa siyo tena kwa ajili ya kumsaidia mwananchi. Kwa mfano, kuna baadhi ya mabasi ambayo ofisi zao ziko Mbagala, Gongo la Mboto, Kariakoo au Urafiki ambayo kabla stendi haijahamishwa kutoka Ubungo kwenda huko, wakati tunasafiri tulikuwa tunawaomba tunapandia huko kwenye ofisi zao, lakini baada ya kuhamia huku kwenye stendi ya Magufuli, wamesema wamekatazwa kutoka na abiria nje ya stendi," alisema mmoja wananchi.

"Yaani hata kama gari ulilopanda linapaki Mbagala na mmefika usiku wa manane Mbezi kwenye hiyo stendi, wanakatazwa wasitoke na abiria wanaokwenda Mbagala, Gongo la Mboto au kwingineko. Sasa hii ni kero na siyo utu, badala ya kuwasaidia wananchi ni kama wanatukomoa." Wengine wanaolalamika ni wafanyabiashara wadogo waliopata vibali vya kufanyabiashara katika stendi hiyo, kukosa wateja baada ya kuruhusiwa wenzao ambao wanaingia bila kibali kwa mgongo wa kwamba hawana mtaji mkubwa na kufanya biashara zao kama kawaida.

Katibu wa wafanyabiashara wenye vibali vya kuendesha shughuli zao katika stendi hiyo, Mohamed Pazi, alisema kwa sasa kinachofanyika katika stendi hiyo katika upande wa biashara ni vurugu.

"Wanajiita kwamba wao hawana mtaji mkubwa, lakini cha kushangaza wanaingia na biashara kubwa kama sisi na wengine wanatuzidi, wanaweka meza zao chini pembezoni mwa eneo ambalo magari yanatumia kupakia abiria, kwa hiyo badala ya sisi tunaolipa kufanya biashara wao ndio wanakuwa wanafanya biashara, hii siyo sawa na hivi tunavyozungumza sisi wenye vibali tuna hali mbaya ya kufilisika hata mitaji yetu."

Ofisa Habari wa Manispaa ya Ubungo, Joina Nzali, alisema suala la mabasi kutoruhusiwa kuingia au kutoka na abiria kwenye stendi hiyo ni utaratibu ambao umewekwa kwa makubaliano ya pamoja kati ya uongozi wa wilaya ya Ubungo na wamiliki wa mabasi wenyewe.

"Huu ni utaratibu ambao ulifikiwa kati ya uongozi wa wilaya na wamiliki wenyewe na hata wale ambao bado ofisi zao za kukatia tiketi ziko ziko nje ya stendi, wamepewa muda kwamba mpaka kufikia jumanne ya wiki ijayo wawe wamehamishia ofisi zao humo, zisiwapo nje ya stendi,"alisema Nzali.

"Ikumbukwe kwamba hii stendi imejengwa kwa fedha, kwa hiyo inatakiwa iingize fedha, sasa mabasi yanapopakia abiria nje ya stendi, mapato si yatakosekana, kwa hiyo abiria wanapoingia na kulipa tozo stendi nayo inapata mapato."

"Na ndiyo maana mtu unaposafiri unakuwa umejiandaa, usitegemee kwamba basi litakupeleka mpaka Mbagala, Gongolamboto au mahala pengine popote eti tu kwa sababu lina ofisi zake huko, kwa sababu pia si muda mrefu mabasi yote yatakuwa na ofisi zake ndani ya stendi." Kuhusu malalamiko ya wafanyabiashara wadogo wasio na vibali, Nzali alisema waliruhusiwa kuingia baada ya amri ya serikali kutaka waruhusiwe.

Kwa upande wao Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania 3(TABOA), kilikiri kupewa masharti hayo ya kutokupakia au kutoka na abiria nje ya stendi.

Pia, alisema wamemwandikia barua Mkuu wa wilaya hiyo ya Ubungo, kujieleza kuhusu baadhi ya maelekezo ambayo wamepewa ili yaangaliwe vizuri kwa upya.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (wa pili kushoto), akisikiliza maelezo kuhusu utendaji wa machinjio ya kisasa katika eneo la Kizota, jijini Dodoma jana, alipofanya ziara ya kikazi kukagua utunzaji wa mazingira. **PICHA: OMR**

# Spika aagiza mjadala sakata hasara ATCL

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema kutokana na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kupata hasara ya Sh. bilioni 60, ni vyema wabunge wakashauri serikali iangalie aidha iendelee kuagiza ndege au ilisitishe kununua hadi mambo yatakapokuwa sawa.

Ndugai alitoa kauli hiyo bungeni jana kabla ya wabunge kuanza kuchangia Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo (2021/22 hadi 2025/26) uliowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Mwigulu Nchemba.

Alisema wabunge wanapochangia Mpango huo washauri serikali kama iendelee na mpango wake wa kununua ndege ama isitishe hadi itakapoweka mambo sawa.

"Ripoti ya CAG ya mwaka 2019/20 tumepata hasara kwa ATCL ya Sh. bilioni 60, je, tukiendelea kuagiza ndege mpya itasaidia au tusimame kidogo kwa sasa zitumike zilizopo na kadhalika, mawazo kama haya ni muhimu kipindi kama hichi," alisema.

Ndugai alisema pia katika ununuzi wa mabehewa kwa ajili ya uendeshaji wa reli ya kisasa ya SGR washauri kama ni vyema yakanunuliwa na Serikali au ununuzi ukafanywa na wabia wa sekta binafsi.

Alisema zipo nchi zinafanya uwekezaji wa miundombinu ya reli na suala la mabehewa linafanywa na wawekezaji binafsi.

**MAONI YA KAMATI**

Kamati ya Bunge ya Bajeti, ilitoa angalizo kuhusu mikopo inayokopwa na serikali kwamba yote ielekezwe katika kukamilisha miradi ya maendeleo hasa ile ya kimkakati iliyoanzishwa badala ya kuanzisha miradi mipya.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Sillo Baran, alisema Deni la Taifa limeendelea kukua na kufikia Sh. trilioni 59 hadi kufikia Desemba 2020.

"Kati ya kiasi hicho deni la ndani lilifikia Sh.trilioni 16.2 na deni la nje Sh. trilioni 42.8, ongezeko la deni limetokana na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo,"alisema.

Alisema kutokana na ukopaji huo kamati hiyo inatoa angalizo kuwa mikopo yote ielekezwe kukamilisha miradi hiyo.

Kuhusu uhimilivu wa deni hilo, alisema katika Mpango huu wa tatu, serikali iendelee kufanya tathmini ya viashiria vyote vya uhimilivu wa deni ili kuona kama vinaendelea kukidhi chini ya viwango vya ukomo vilivyokubalika kimataifa ili liendelee kuwa himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

Kuhusu usafiri wa anga, Mwenyekiti huyo alisema kamati inaishauri ATCL kuongeza safari zake za ndani ili kujiongezea miruko na hivyo kupunguza hasara kwa kusimamisha ndege.

"Aidha, ATCL itumie fursa ya kusafirisha mizigo hasa matunda, mboga, maua na samaki kutoka hapa nchini kwenda nchi za nje badala ya kuachia ndege za nchi jirani kutumika,"alisema.

# Waziri aingia matatani bungeni

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, ana majibu ya ovyo, hivyo amemshauri Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kumfunda namna ya kujibu hoja za wabunge.

Ndugai alitoa kauli hiyo bungeni jijini hapa jana muda mfupi baada Mbunge wa Singida Magharibi, Elibariki Kingu (CCM) kulalamikia kuhusu majibu ya waziri huyo.

Kingu alitoa malalamiko hayo alipochangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 hadi 2025/2026), na kuwataka mawaziri waache kuwaona wabunge wanaowashauri ni maadui.

Alisema alimweleza Mwambe kuwa Watanzania wana tatizo kwenye masoko, lakini alimjibu vibaya kwamba aseme tu kama nyama anayouza imekosa soka, majibu ambayo alidai yalimkwaza. "Mimi ni mbunge, ni mwakilishi wa watu, we are doing this for interest (tunafanya hivyo kwa maslahi) ya nchi, jibu alilonipa 'kama nyama yako imekosa soko', mimi siuzi nyama," alisema, na kuongeza anazungumza kwa niaba ya wafanyabiashara na si maslahi yake binafsi. Alisema mawaziri pia wanapaswa kuacha kufikiri wabunge wanaposhauri, wametumwa na wafanyabiashara bali wanafanya hivyo kwa maslahi ya nchi.

Kutokana na malalamiko hayo, Spika Ndugai alisimama na kusema amepokea malalamiko ya aina hiyo dhidi ya Mwambe kutoka kwa wabunge kuhusu majibu ya ovyo na ya kifedhuli anayoyatoa.

"Ninayo malalamiko kadhaa kuhusu Waziri Mwambe. Ninadhani kwa sababu ni mbunge mgeni, anadhani kuwa ukiwa waziri ni mtu mkubwa sana bungeni, haiendi hivyo.

"Ana majibu ya ovyo sana, hawaheshimu hata wabunge wa kamati yake, wanapata tabu jinsi ya kufanya naye kazi," alisema.

Alisema japokuwa ni mgeni na ndiyo anaanza kazi na kwa bahati nzuri Rais Samia Suluhu Hassan amemwamini, anafikiri Mwambe hajajua nafasi ya wabunge katika wizara yake na shughuli zake.

"Haiwezekani! Ukimnyanyasa mbunge mmoja, umenyanyasa wabunge wote, ukinyanyasa kamati moja, umenyanyasa kamati zote. Duniani kote hakuna waziri anayemjibu fedhuli mbunge, ni vizuri tumwachie Mheshimiwa Waziri Mkuu ili akakae naye amfunde.

"Bado mgeni, kwa sasa hivi tumsamehe, hata wabunge wa mkoani kwake Mtwara haelewani nao wote huyu na ni ufedhuli huo huo. Kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu akalifahamu," alihitimisha Spika Ndugai.

## TANGAZO


# MINIMUM DISCLOSURE OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

NMB
Karibu yako

| S/N | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | **SAVINGS ACCOUNTS** | |
| | Required minimum opening balance | Business saving A/C TZS 100,000, USD 100,EUR 100,GBP 100; Bonus A/C TZS 50,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Mtoto A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Chipukizi A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Pamoja A/C TZS 30,000 |
| | Transaction fee | N/A |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | FREE |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 4,000 for amount up to TZS 5Million; TZS 4,000plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Withdrawal bulky without notice | OTC: TZS 4,000 for amount up to TZS 5Million; TZS 4,000plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Savings Card/Passbook | N/A |
| | Passbook/Card Replacement | TZS 11,800 |
| | Closing Account | TZS 9,440 USD 11.8, EUR 11.8 & GBP 11.8 |
| 2 | **CURRENT ACCOUNT** | |
| | Required minimum opening balance | Business, Supply Chain, Trade Business, Agribusiness Overdraft, Agribusiness Loans, Agri-General, Corporate, Emerging Corporate A/C - TZS 100,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Personal A/C - TZS 15,000; Mwanachuo & Chapchap A/C - TZS 10,000; Wisdom - FREE; Group A/C - TZS 30,000; Fanikiwa A/C - TZS 20,000; Exclusive A/C - TZS 1Million; Executive A/C - TZS 500,000; Kilimo & Bonus A/C - TZS 50,000; Float & Scheme Financing A/C - FREE; Notice Investment A/C - TZS 500Million;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- ZERO |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | Personal A/C - TZS 1,800; Business A/C & Agribusiness - TZS 15,340; Corporate, Insitution & Trade Business A/C - TZS 19,200; Exclusive A/C - TZS 35,400; Executive A/C - TZS 23,600; Emerging Corporate - TZS 19,200; Fanikiwa - TZS 2,000; Personal A/C Agribusiness - TZS 2,048; Kilimo is - TZS 1,800; for Forex A/C charges are Equivalent to TZS;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- FREE |
| | Transaction fee | N/A |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Bank Drafts | NA |
| | Bank Drafts cancellation charge | NA |
| | Cheque book (100 leaves) | TZS 48,380 USD 35.4, EUR 23.6 & GBP 17.7 |
| | Cash Withdrawal at Counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Special Clearance | TZS 53,100 USD 52.8, EUR 46 & GBP 39.5 |
| | Cheque withdraw over the counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Dishonoured cheque | 1.5% of the amount Min 64,000 Max TZS 118,000 |
| | Cash Payment to 3rd party | N/A |
| | Cash Deposit Charge | N/A |
| | Overdrawn account interest charge | N/A |
| | Unarranged Overdraft | N/A |
| | Bulk cash Deposit | FREE |
| | Bulk cash Withdrawal | N/A |
| | Stop Payment orders | TZS 35,400, USD 23.6, EUR 17.7 & GBP 17.7 |
| | Standing Orders ( within the same bank) | FREE |
| | Standing Orders ( to other bank) | TZS 19,710 |
| | Letter of introduction | N/A |
| | Salary handling | TZS 3,540 |
| | School fees deposits | FREE |
| | TRA collection | FREE |
| | Safe custody charges | N/A |
| | Safe custody access fees | N/A |
| 3 | **EFT** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | FREE |
| | To other Banks ( On Others) | 2000 |
| (b) | Outward Transfers | 2000 |
| | Inward Transfers | FREE |
| 4 | **TISS** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | N/A |
| | To other Banks ( On Others) | TZS 10,000 |
| (b) | Outward Transfers | TZS 10,000 |
| | Inward Transfers | FREE |

| 5 | FOREIGN EXCHANGE ACCOUNT | Savings Acc | Current Acc |
|---|---|---|---|
| | Transaction fee | N/A | N/A |
| | Statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | |
| | Interim statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | USD1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month |
| | Withdrawal Charges | 0.25% of the amount - forex | 0.25% of the amount - forex |
| | Cash Deposit Charge | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) |
| | Purchase/Sale of TC transactions over the counter | N/A | N/A |
| | Purchase of Foreign Cheque | N/A | N/A |
| | Sale/ Purchase of cash passport | N/A | N/A |
| | Telex/SWIFT | USD 58 | USD 58 |
| | Transfer from foreign currency denominated account to local account | N/A | N/A |
| | Outward foreign transfers | USD 58 | USD 58 |
| | Inward foreign transfers - Customers | FREE | FREE |
| 6 | **ATM CARD AND TRANSACTIONS RELATED** | | |
| (a) | Local Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | N/A |
| (b) | International Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - FREE; World Reward - FREE |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| (c) | ATM Withdrawals: | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | From TZS 1,100 - 1,500 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | TZS 3,540 |
| | ATM mini statement | N/A | TZS 413 |
| | Bill payments through ATM | N/A | FREE |
| (d) | POS | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | TZS 1,770 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | FREE |
| 7 | **MOBILE (SMS) BANKING** | | |
| | Balance Inquiry | N/A | TZS 400 |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers (within NMB) | N/A | FREE |
| 8 | **INTERNET BANKING** | | |
| (a) | Domestic: | | |
| | Balance Inquiry | FREE | FREE |
| | Payments | TZS 640 | TZS 640 |
| (b) | International | | |
| | Balance Inquiry | N/A | FREE |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers | N/A | USD 45 |
| 9 | **MONEY REMITTANCES** | | |
| (a) | Western Union | | |
| | Sending | N/A | N/A |
| | Received | N/A | N/A |
| (b) | Money Gram | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (c) | Coinstar | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (d) | Travelex | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (e) | Africash | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (f) | Others (Specify) | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |

| 10 | BANKING SECTOR - DEPOSITS & LENDING RATES | | |
|---|---|---|---|
| A | TYPES OF LENDING RATES | LENDING RATES - PA (%) | |
| | | TZS | USD |
| (a) | Flat | | |
| (b) | Declining | 17% | 9% |
| (c) | Negotiable | | |

**B FIXED DEPOSITS**

| PERIOD | TZS | | | USD | GBP |
|---|---|---|---|---|---|
| | 500K><9.9Mil | 10M><99.9M | 100M><199M | 2000-49,999 | 2000-49,999 |
| I Month | 2.00% | 2.25% | 2.50% | 0.45% | 0.25% |
| 2 Months | 2.50% | 2.75% | 3.00% | 0.55% | 0.30% |
| 3 Months | 3.00% | 3.25% | 3.50% | 0.70% | 0.40% |
| 6 Months | 3.50% | 4.00% | 4.50% | 0.80% | 0.50% |
| 9 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 12 Months | 5.00% | 6.00% | 7.00% | 1.00% | 0.60% |
| 13-24 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 25-36 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |

**Signed By:**

Aloyse Maro
Head Retail Products & Channels

Filbert Mponzi
Chief Retail Banking




*Vigezo na Masharti kuzingatiwa.

www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Haya yafanyiwe kazi TRA kuongeza mapato

**APRILI** 6, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, alirudia agizo lake kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuacha kuwanyanyasa wafanyabiashara na wawekezaji, jambo ambalo limefukuza wengi kwenda kuwekeza katika nchi nyingine duniani.

Aidha, alionyesha kusikitishwa na ubabe, uporaji unaofanywa na maofisa hao ambao walikuwa kwenye kikosi maalum, ambacho kiligeuka kufanya dhuluma kwa wafanyabiashara.

Rais Samia alisema zaidi kwamba hatahitaji kodi ya dhuluma na kama watakusanya kodi ya dhuluma, ni heri wasikusanye kwa kuwa siku zote dhuluma haina safari ndefu, na siyo haki mbele ya Mungu.

Vitabu vitakatifu vimesema ya Kaisari (dola) mpe Kaisari na ya Mungu mpe Mungu, yaani inatambulika kodi na ada mbalimbali za kisheria ni kwa wahusika, huku Mungu yake ni fungu la kumi, zaka, sadaka ya malimbuko, sadaka ya amani na nyinginezo ambazo zimetajwa. Kilio cha wafanyabiashara kimekuwa kikubwa kwa kuwa ilifikia mahali wengi kuonekana ni wezi, wapigaji na kodi za nyuma kutumika kama fimbo ya kuwachapa, kiasi kwamba wengi wamefilisika.

Athari za yaliyokuwa yanafanyika ni wafanyabiashara kuondoa fedha benki na kuzificha nyumbani, kwa kuwa kila walivyoonekana na kiasi fulani benki zilichukuliwa na kushindwa kujiendesha, jambo ambalo ni baya. Wafanyabiashara hawa wenye uwekezaji katika maeneo mbalimbali nchini walifunga shughuli zao, hivyo kusababisha Watanzania wengi walioajiriwa kwenye sekta binafsi kupoteza ajira na mzunguko wa fedha kupungua.

Rais Samia ameliona tatizo na kutoa maelekezo ya kulishughulikia ili kurudisha fedha kwenye mzunguko na kujenga imani kwa jumuiya ya wafanyabiashara na sekta binafsi kwa ujumla.

Hakuna ubishi kuwa kampuni na biashara nyingi zimefungwa, na siyo kwa kupenda bali mazingira yalikuwa yenye kuumiza na kutishiwa kubambikiwa kesi za uhujumu uchumi na hata maisha yao.

Tunaamini kwa mabadiliko ya uongozi ambayo Kamishana Mkuu wa sasa, Alphayo Kidata, ambaye alishapita TRA, kutakuwa na nuru njema na sasa watu watafanya biashara na kulipa kodi zote muhimu kwa mujibu wa sheria. Lakini tunakifiri haitoshi kushughulikiwa suala hili bila kwenda kwenye mzizi wa tatizo, kwa kuangalia upya sheria za kodi na uanzishaji biashara, ambazo zimelalamikiwa kwa muda mrefu na hata Ripoti ya Hali ya kufanya Bishara Tanzania inayotolewa na Benki ya Dunia (WB), imeainisha vikwazo mbalimbali.

Kuvunja kikosi kazi na kukemea ubabe, unyang'anyi na dhuluma nyingine haitoshi, maana ni sawa na kutibu kidonda kwa juu wakati ndani bado hakijapona, bali tunashauri kinachotakiwa kufanyika ni kupitia upya sheria mbalimbali ambazo ni tatizo kubwa.

Ukuaji wa biashara utaongeza ajira kwa wingi na kupunguza wategemezi na wasio na ajira, ambao wangeingia kwenye wizi na shughuli nyingine zisizo halali.

Kiwango cha ajira kimeendelea kupungua kila siku, na hao hao wanaotarajiwa kulipa kodi walibanwa kiasi cha kufilisika, hali ambayo ilikuwa ni yenye mafinikio makubwa kwa muda mfupi lakini siyo endelevu. Tunampongeza rais kwa kuliona hilo, lakini bado tunamuomba jicho lake limulike kila mahali na sasa tuone ujenzi wa sekta binafsi imara ambayo itakuwa na nguvu ya kuajiri mamia ya wananchi ambao sasa wako mtaani licha ya kuwa na utaalamu mwingi.

Serikali yoyote inayotaka kufanikiwa katika kukusanya kodi huimarisha sekta binafsi kwa kujenga mazingira wezeshi na siyo kuiua, kwa kuwa hakuna ubishi kuwa serikali haiwezi kuajiri wala kutengeneza ajira nyingi. Itakuwa ni hujuma kama viongozi wa serikali watakuwa na fikra kuwa serikali inaweza kufanyakazi yenyewe kwa yenyewe na haihitaji sekta binafsi, jambo ambalo huko nyuma lilishindikana kwa kuwa mashirika na viwanda vingi vya umma kama Kiwanda cha General Trye vilikufa, lakini usimamizi na uendeshaji wa sekta binafsi ulifufua na kuleta tumaini la maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Halmashauri ziboreshe masoko waliko Machinga, ili kumuenzi Hayati JPM

Na Sabato Kasika

**SIKU** 21 za maombolezo ya msiba mkubwa uliolikumba taifa kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais Dk. John Magufuli zimeisha na sasa Watanzania wanaendelea na kazi ya kujenga taifa lao.

Pamoja na hayo, ipo haja ya kukumbushana yale ambayo Hayati Dk. Magufuli wakati wa uhai wake, alikuwa hataki kuyaona, ikiwamo kuhamisha ovyo wamachinga bila ya kutengewa masoko rasmi ya kufanyia biashara.

Kutokana na hali hiyo, aliwahi kumuagiza Waziri na Katibu Mkuu katika Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kusitisha utekelezaji wa mpango wa kuwaondoa katika jiji la Mwanza na mikoa mingine.

Dk. Magufuli alitoa agizo hilo Desemba mwaka 2016, ili kuhakikisha kwanza mamlaka husika zinakamilisha maandalizi ya masoko ambayo watahamishiwa badala ya kuwatimua tu kuwaacha wakihangaika.

Alionya kuwa kiongozi yeyote ambaye hayupo tayari kutekeleza agizo hilo aachie ngazi na kuziagiza halmashauri na manispaa, kuboresha masoko yaliyopo kuyawekea miundombinu yote muhimu ikiwamo maji, vyoo na huduma nyingine na kujenga mapya ndipo wahamishwe.

Hata hivyo, hadi anafariki dunia mwasisi huyo wa wazo, Wamachinga bado wanaendelea kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi, hali inayoonyesha, maagizo yake hayakutekelezwa.

Kwa kuwa mwenyewe sasa ametangulia mbele za haki, ingependeza viongozi wa halmashauri mbalimbali, ziwe manispaa, jiji au halmashauri ndogo na za wilaya, manispaa zimuenzi kwa kuboresha masoko ya wamachinga waondoke kwenye maeneo yasiyo rasmi.

Ikumbukwe kuwa, hivi sasa ni miaka minne na ushee tangu agizo hilo litolewe, lakini bado wamachinga wameendelea kutapakaa katika mitaa kwenye miji mbalimbali nchini wakiendelea na biashara.

Dk. Magufuli alionyesha kujali kundi hilo hadi kufikia kulikabidhi vitambulisho maalum, na pia alitamani kuona linaboreshewa mazingira ya kufanyia biashara ili liache kutangatanga huku na kule.

Muungwana anaamini kwamba, njia mojawapo ya halmashauri na manispaa kumuenzi Hayati Dk. Magufuli, ni kutenga maeneo rasmi ya kufanyia biashara, lakini yakiwa yameboreshwa kama alivyotamani yawe.

Iwapo mamlaka husika zitamuenzi kwa kuboresha masoko ya wamachinga, zitakuwa zimesaidia kuwaondoa katika maeneo hatarishi ambayo wamekuwa wakiyatumia kufanya biashara zao za kila siku.

Ni wazi kwamba, Wamachinga wengi wanafanya biashara zao kwenye maeneo ya hatari kama chini ya nyaya za umeme mkubwa na kando ya barabara, mazingira ambayo kwa ujumla si salama kwao.

Kwa kuwa mamlaka husika zilishaagizwa kuwahamisha wamachinga iwapo tu zitakuwa zimewatengea maeneo mengine ambayo ni wa rafiki kwa shughuli zao, basi ingefaa zitekeleze maagizo hayo.

Hatua hiyo, pia itasaidia kupunguza tatizo la uchafuzi wa mazingira ambao umekuwa ukifanywa na Wamachinga, baadhi yao wanatupa taka wanazozalisha, katika mitaro ya maji ya mvua.

Kama viongozi wa mamlaka husika hasa wa jijini Dar es Salaam wamewahi kuzungukia maeneo yao, watakuwa wameshuhudia jinsi ambavyo wamachinga wanafanya biashara ndani ya mitaro na maeneo mengine.

Rais Dk. Magufuli amefariki, ilhali maagizo yake katika halmashauri hayakutekelezwa. Nashauri kuanza na hilio Machinga.

Iwapo hayo yatafanyika, mandhari ya jiji la Dar es Salaam itaonekana kwa uasili wake. Binafsi ninaamini, hatua ya Dk. Magufuli kutaka wamachinga wasisumbuliwe, ilitokana na kuwaona ni watu wenye changamoto nyingi katika jamii ikiwamo elimu duni na ukosefu wa ajira, hivyo wanahitaji kusaidiwa.

Hivyo, hatua ya kutaka waboreshewe masoko kwanza kabla ya kuondolewa katika maeneo waliopo sasa, ilionyesha kuthamini mchango wa wamachinga katika kukuza uchumi wao na pato la taifa.

Kwa hali hiyo, umuhimu wa kuwatengea maeneo yao yakiwa yameboreshwa, kama ambavyo Hayati Dk, Magufuli alikuwa akitaka, ni jambo la muhimu na mamlaka husika zikitekeleza hilo zitakuwa zimemuenzi.

# TANGAZO

## RE-ADVERTISEMENT

### PREQUALIFICATION OF VENDORS FOR PROVISION OF VARIOUS SERVICES FOR NMB BANK PLC. FOR THE YEAR 2021/2022

NMB
Close to you

### Invitation to Tender

1. NMB Bank Plc. (the **"Bank"**) is the largest commercial Bank in Tanzania in terms of branch network, customer base and profitability. NMB is committed to sustaining and enhancing the branch network in order to provide access to financial services to citizens in all areas of Tanzania, with special focus on rural areas;

2. The Bank has set funds for the year 2021, towards the cost of operations and maintenance of its facility for NMB HQ and its Branch network. It is intended that part of these funds will be applied to eligible payments under the contract (s) for provision of various services to the Bank;

3. The NMB Bank Plc. Management Tender Committee now invites all eligible, qualified and competent vendors to submit their applications for prequalification of vendors for provision of various services for the Bank as detailed in the below list;

**List of various services for NMB Bank Plc. for the Year 2021**

| SN | Description of Services |
|---|---|
| 1 | Building Contractors Class 1 to 7 |
| 2 | Architectural Consulting Services for Various NMB Projects |
| 3 | Consulting Quantity Surveyors (QS) for Various NMB Projects |
| 4 | Engineering Consulting Services for Various NMB Projects |
| 5 | Provision of Structural Engineering Consulting services |
| 6 | Consulting Quality assurance (QAs) for Various NMB Projects |
| 7 | Provision of Data Cabling works |
| 8 | Provision of Physical Security Specialty Services |
| 9 | Supply of Stationeries |
| 10 | Office Equipments (Facilities) |
| 11 | Furniture and Furnishings |
| 12 | Installation, Service & Maintenance of Fire Detection & Alarm System |
| 13 | Travel Agency Services |
| 14 | Supply and installation of Blinds Curtains |
| 15 | Clearing & Forwarding Agents |
| 16 | Supply & Service of Strong Room Doors |
| 17 | Asset Valuation and Fixed Asset Management Solution |
| 18 | Supply of Electrical Equipments and Appliances |
| 19 | Borehole Drilling and Pump Installation Services |
| 20 | Guarding and Response Services |
| 21 | Supplying Tropical Fresh Flowers for Offices |
| 22 | Supply of Mobile Phones |
| 23 | Provision of Auditing and Tax Advisory Services |
| 24 | Disposal of Hazardous Equipment |
| 25 | Supply of Motor vehicles |
| 26 | Provision of Branding and Signage for Dar and upcountry |
| 27 | Provision of Printing Services for Dar and Upcountry (Fliers, Posters, Brochures, Calendars) |
| 28 | Supplying of Various Promotional Materials(T-shirts, Caps, Thermal Mugs, executive pen, Plastic pen, etc. |
| 29 | Provision for events and experiential services for Dar and upcountry |
| 30 | Provision of Digital and social Media Services |
| 31 | Provision of Various Research Services |
| 32 | Provision of Translation and Copyright Services |
| 33 | Provision of Radio, Jingle and IVR Production |
| 34 | Provision of Creatives, Concepts and Designing for Campaigns |
| 35 | Provision of Photography Services |
| 36 | Provision of TVC and Video Production Services |
| 37 | Provision of Interior Designing and Decoration Services for NMB Premises |
| 38 | Supplying of Hospital Equipments |
| 39 | Supplying of Sports gears |
| 40 | Supply of staff uniform |
| 41 | Supplying of Building and Roofing Materials for Dar and Upcountry |
| 42 | Supplying of school Desks (for Donation Services) |
| 43 | Provision of Hotel Conference Services and Venue Hiring |
| 44 | Provision of Political and Economic Analysis (PEA) and stakeholder mapping services |
| 45 | Vendors for Social Media Influencers |
| 46 | Vendors for Provision of Catering & Drinks Services |
| 47 | Vendors for Courier Services |
| 48 | Provision of HR Consulting services (permit and visa follow up etc.) |
| 49 | Provision of wellness services |
| 50 | Supply, service and maintenance of Office Equipment - Safes, Shredders, strapping machine |
| 51 | Supply and Installation of Shelves for Storage Purposes |
| 52 | Supply of Teller Cash Boxes, cash in transit boxes |
| 53 | Electrical systems Contractors |
| 54 | Contractors for provision of cooling systems and maintenance |
| 55 | Provision of Network Passive connectivity services (Provision of Structural and Data Cabling works) |
| 56 | Supply of ICT Hardware and software |
| 57 | Provision of data and voice services |
| 58 | ICT Consultancy services (Design, Health check, Support, Development, ICT Audit, Deployment, etc.) |
| 59 | Contractors for fire detections and suppressions |
| 60 | Supply of Network Active equipment's (Routers/Switches, Firewalls, LB, etc.) |
| 61 | IT Service Management |
| 62 | Supply of ICT Equipments (Computers, Printers and Scanners etc.) |
| 63 | Supply, Installation and Servicing of Generators |
| 64 | Supply of SMS Services |
| 65 | Supply of ICT Consumables/Peripheries (Mouse, adapters, keyboards etc.) |
| 66 | Vendors for Provision of Printing services |
| 67 | Vendors for Provision of Printing cheque books |
| 68 | Vendors for Provision of Car tracking and fuel monitoring services |
| 69 | Supply of tyres and fitting services |
| 70 | Vendors for Provision of Service and Maintenance of Vehicles |
| 71 | Supply of Petroleum products |
| 72 | Vendors for Provision of Tours and Travel |
| 73 | Vendors for Provision of Accommodation Services (Hotels and apartments in Dar) |
| 74 | Supply of Bank Financial Cards (EMV Cards) |
| 75 | Vendors for Provision of Legal Services |
| 76 | Distributors of Air Conditioners |
| 77 | Vendors for supply of construction materials across NMB Network (e.g. cements, roofing and plumbing materials) |
| **Provision of Various Training services in the following categories** | |
| 78 | Leadership Program |
| 79 | Operations and Risk Management |
| 80 | Fraud |
| 81 | Risk & Controls |
| 82 | Bancasurance |
| 83 | Trade Finance |
| 84 | Business Communication Skills |
| 85 | Customer Experience training |
| 86 | Credit |
| 87 | Sales training |
| 88 | IFRS Update |
| 89 | Regulatory Reporting : Bank of Tanzania Regulations |
| 90 | Due Diligence and Supplier relationship management |
| 91 | National Payment System, |
| 92 | National Switch |
| 93 | TACH |
| 94 | PMP Training and Certification |
| 95 | Cyber Laws |
| 96 | Negotiation |
| 97 | Loan recovery/Collection and Monitoring |
| 98 | Data Centre management |
| 99 | Prudential Regulations Trainings |
| 100 | Cyber Crime Investigation |
| 101 | Agri-business |
| 102 | Records Management |
| 103 | Conflict Resolution |
| 104 | Pre-Retirement Training |
| 105 | Team Building |
| 106 | Islamic Banking |

4. This is re-advertisement, therefore those who submitted their application in the first round and have received email notification for being successful, does not need to apply.

5. The Selection of eligible and qualified vendors in respective services will be conducted through Open Competitive Tendering Procedures as specified in the NMB Bank Plc. Procurement Policy and Procedures;

6. The selection Criteria will include:
   - Possession of registration certificate from relevant authorities, business license, company certificate of incorporation, TIN, VAT Registration.
   - The company must have not less than three years' experience in the relevant field, complexity in different organizations.
   - Submit the list of key staff with their CVs demonstrating their ability to carry out the applied service.
   - Current physical location (which will be inspected for verification); that is a valid right of occupancy of office premises or lease contract
   - Submission of power of attorney document
   - Submission of certified declaration on Litigation information regarding your firm.
   - Submission of three years audited financial statements i.e. 2017, 2018 and 2019

   Please note that in assessing the submissions, consideration will be given to the qualifications, experience on similar assignments and capacity to undertake the applied assignment. Only eligible and qualified Companies with demonstrated experience and excellent track records in similar assignments will be considered.

7. Deadline for submission of the documents is **Tuesday 20th April 2021 at 15.00HRS**. Applications will be opened promptly thereafter in public and in the presence of bidder's representatives who will choose to attend the meeting.

8. Applicants must include one original and a copy of their tender document. The documents must be properly filled and enclosed in plain envelopes clearly marked **"Prequalification for Provision of (Put the name of the selected service) – Not to be opened before Tuesday 20th April 2021 at 15.00HRS"** hand-delivered or courier to NMB Bank Plc. through addresses provided below.

9. Late applications, portion of applications, electronic applications and applications not received, opened and read out in public at the tender opening ceremony shall not be considered for evaluation irrespective of circumstances.

**The Chief Executive Officer**
**P.O. Box 9213, Dar es Salaam, Tanzania.**
**NMB Bank Plc. Head Office Ohio/Ali Hassan Mwinyi Streets**

*www.nmbbank.co.tz*

## Mabilioni ya NSSF yalivyopotea

**Na Salome Kitomari**

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ( CAG) imeonyesha kuwa kampuni tanzu ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), imetengeneza hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 4.72 kwa mwaka 2019/20 kupitia uwekezaji uliofanyika katika viwanda vya kuzalisha sukari vya Mbigiri na Mkulazi.

Aidha, NSSF imeshindwa kukusanya kiasi cha Sh. bilioni 28.8 ambazo zilitolewa kama mikopo kwenye Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS), vipatavyo 134 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020.

"Nilibaini kuwa, vyama 14 vilivyokopeshwa Sh. bilioni 14 havifanyi marejesho ya mikopo. Hali hii inasababisha hasara kwa NSSF na ukosefu wa fedha za kugharamia kazi zingine," ilisema ripoti hiyo.

Katika ukaguzi wa ufanisi juu ya utekelezaji wa mradi wa uzalishaji wa sukari Mbigiri walibaini kuwa mbolea na dawa za kuulia wadudu zenye thamani ya Sh. 241,889,000 zilitolewa ghalani ila hapakuwa na maelezo ya namna ambavyo mbolea hii ilitumika.

Alisema miwa iliyopita muda wake wa mavuno ilionekana katika vitalu mbalimbali kwenye shamba la Mbigiri ikiwa imeharibika na kupoteza thamani yake ya kiuchumi.

Pia, makisio ya hasara iliyotokana na gharama za uzalishaji wa miwa hiyo ni kiasi cha Sh. 379,338,245. CAG alibainisha kuwa visima vinne katika shamba la Mbigiri kitalu E3, D2, E4 na F4 vilichimbwa lakini havitumiki kwa sababu havina uwezo wa kutoa maji ya kutosha kwa shughuli za umwagiliaji.

"Pia, nilibaini kuwa mkandarasi aliondoka eneo la kazi licha ya kuwa alishalipwa Sh. 81,500,000 sawa na asilimia kumi ya gharama zilizoainishwa kwenye mkataba," alisema.

Alisema kampuni ya Mkulazi ilishindwa kusimika mtambo wa kuchakata sukari kwa wakati na kusababisha benki ya Azania kusitisha kutoa mikopo kwa wakulima wa nje kiasi cha Sh. 1,797,050,000 ambazo zingewawezesha wakulima hao kukidhi gharama mbalimbali za kuzalisha miwa.

"Tangu kuanzishwa kwake Kampuni ya Mkulazi haijasajiliwa kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani. Kampuni iliingia mikataba 52 yenye thamani ya Sh. 50,279,515,851.70 na mikataba hiyo imejumuisha kodi ya ongezeko la thamani yenye kiasi cha Sh. 7,669,756,655.34 katika mwaka wa fedha 2017/18 to 2019/20 ambazo zingeweza kutumika kwa shughuli nyingine,"ilifafanua ripoti hiyo.

CAG alisema Kampuni Hodhi ya Mkulazi ilimlipa mkandarasi kiasi cha Sh. 397,020,000 kama malipo ya maandalizi bila kuwa na vielelezo vya vipengele vilivyolipwa.

# Tril. 114/- kutumika, mpango maendeleo miaka mitano ijayo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewasilisha bungeni mpango wa tatu wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano ambao utagharimu Sh. trilioni 114.8, huku ikiweka wazi miradi itakayotekelezwa kwa kipindi hicho.

Fedha za mpango huo wa mwaka 2021/22 hadi 2025/26, zimeongezeka kwa Sh. trilioni 7.8 ikilinganishwa na mpango wa pili uliopita wa 2016/17 hadi 2020/21 ambao ulikadiriwa kutumia Sh. trilioni 107.

Mpango huo, unalenga kuipa sekta binafsi uzito mkubwa huku ukipendekeza utekelezaji wa miradi ya kielelezo ikiwamo Mradi wa Kufua Umeme wa Maji - Julius Nyerere MW 2,115, kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa.

Akiwasilisha jana bungeni mpango huo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alitaja miradi mingine kielezo kuwa ni makaa ya mawe, Mchuchuma na Chuma Liganga ikijumuisha ujenzi wa reli ya kiwango cha Kimataifa (SGR) kutoka Mtwara hadi Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga.

"Bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania), mradi wa Kuchakata Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) mkoani Lindi, Mradi wa Kufua Umeme wa Maji - Ruhudji MW 358; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji - Rumakali MW 222, uchimbaji wa madini ya Nickel.

"Ujenzi wa madaraja makubwa na barabara za juu za daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza), Tanzanite (Dar es Salaam) na Interchange ya Kamata (Dar es Salaam), Bandari ya Uvuvi (Mbegani) na ununuzi wa Meli za Uvuvi, Kiwanda cha Sukari Mkulazi, Utafutaji wa mafuta katika vitalu vya Eyasi Wembere na Mnazi Bay North, Mradi wa Magadi Soda- Engaruka na kuongeza rasilimali watu yenye ujuzi adimu na maalum," alisema.

**MAMBO YA KUZINGATIWA**

Nchemba alisema miongoni mwa mambo yatakayozingatiwa kwenye mpango huo ni kuhimili athari za majanga ya asili kama vile mafuriko na magonjwa ya mlipuko.

"Ushiriki mpana wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi, hali nzuri ya hewa itakayowezesha uzalishaji wa chakula cha ziada na kuimarika kwa uchumi

wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya kimataifa," alisema.

Alisema pia kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa mwaka kuongezeka kutoka asilimia 6.0 mwaka 2021 na kufikia wastani wa asilimia 8.0 ifikapo mwaka 2026.

"Mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri kuongezeka kutoka asilimia 15.9 ya Pato la Taifa mwaka 2021/22 hadi asilimia 16.8 mwaka 2025/26," alisema.

Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika kipindi cha muda wa kati.

"Akiba ya fedha za kigeni kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne na sekta binafsi kuzalisha ajira mpya zipatazo milioni nane kati ya Julai 2021 na Juni 2026," alisema.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba akiwasilisha mpango wa tatu wa maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2021/2022-2025/2026, bungeni jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Mkufunzi matatani tuhuma rushwa ya ngono

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MKUFUNZI wa Chuo cha Kilimo Maruku, Bukoba mkoani Kagera, Ruta Kyaragaine, anashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa tuhuma za kuomba rushwa ya ngono kwa mwanachuo wa kike ambaye (jina limehifadhiwa) ili amsaidie kufaulu mitihani.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Kagera, John Joseph, alisema Kyaragaine (59) amekuwa akimtisha mwanachuo huyo tangu mwaka jana kuwa asipomkubalia atasababisha asifaulu mitihani.

"Baada ya kupokea taarifa hii, tulianza uchunguzi na Aprili 3, mwaka huu. Tulimkamata mtuhumiwa akiwa katika nyumba moja ya kulala wageni iliyoko katika manispaa ya Bukoba (jina linahifadhiwa) akiwa na mwanachuo huyo akimlazimisha na kumtishia kuwa asipokubali hatamaliza masomo yake," alisema Joseph.

Alisema uchunguzi dhidi ya tuhuma hizo uko katika hatua za mwisho na kwamba ukikamilika atafikishwa mahakamani wakati wowote kuanzia sasa.Mkuu huyo wa TAKUKURU alitumia fursa hiyo kutoa wito kwa wananchi wote mkoani Kagera kupinga rushwa ya ngono kwa kuwa inadhalilisha utu wa mwanamke na kwamba inaweza kusababisha kuambukizwa magonjwa na hatimaye kifo.

"Niwaombe wananchi wote mkoani hapa washirikiane na TAKUKURU na serikali katika mapambano dhidi ya rushwa ya ngono. Pamoja na athari nyingine, husababisha uvunjifu wa haki za binadamu, pia huwafanya wananchi kukosa imani na serikali yao na kudhoofisha maendeleo" alisema.

## Kilichombeba Mo Dewji

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

SIKU moja baada ya mfanyabiashara Mohamed Dewji, maarufu Mo, kualikwa na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, kuingia kwenye jopo la washauri wake katika masuala ya kiuchumi, wabunge wametaja wanachoamini kimembeba bilionea huyo kijana barani Afrika.

Juzi, Mo Dewji anayemiliki Kampuni ya Mohamed Enterprises Limited (MeTL), aliithibishia Nipashe kupata barua kutoka kwa Rais Ramaphosa akimwalika kuingia kwenye jopo hilo.

Akizungumza na Nipashe bungeni mjini hapa jana, mbunge wa Kinondoni, Abbas Tarimba, alisema kuaminika kwa Mo Dewji katika nchi mbalimbali barani Afrika alikowekeza, kumembeba kuingia kwenye jopo hilo la Ramaphosa.

"Mo Dewji amewekeza katika nchi mbalimbali Afrika Mashariki na Kati. Huko kuaminika kwake katika nchi hizo, ninaamini ndiyo siri ya kuonekana kwake kwa Rais Ramaphosa," alisema.

Ahmed Shabiby, Mbunge wa Gairo, alisema anaamini uhusiano wa kibiashara uliopo kati ya kampuni za Mo Dewji na Afrika Kusini umechangia mfanyabiashara mwenzake huyo kualikwa kwenye jopo la washauri wa Rais wa taifa hilo.

Mbunge wa Wawi, Ahmed Juma Ngwali, alisema: "Mo ni mfanyabiashara mkubwa. Ameweka maeneo mengi Afrika Mashariki na Kati. Wenzetu huko wamemuona anafaa kuwashauri, sisi hapa bado."

Ujumbe wa Mo Dewji kwenye jopo hilo utadumu kwa miaka mitano, ukitoa taswira ya Rais Ramaphosa kuthamini mchango wa uwekezaji ambao Mo Dewji ameufanya na kuchochea ukuaji wa uchumi katika nchi mbalimbali barani Afrika ambako kampuni zake zimewekeza na kutoa ajira nyingi.

Mo Dewji alisema juzi kuwa Rais Ramaphosa kupitia barua yake hiyo, amemwalika kuwa mjumbe kwenye Baraza la Ushauri la Rais kuhusu Uwekezaji, ambalo lina jukumu kubwa la kuhakikisha nchi hiyo inapiga hatua kiuchumi kwa kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi hiyo.

Alisema kuwa kiongozi huyo wa Afrika Kusini ameonyesha imani kubwa kwake kuongeza nguvu kwenye mikakati ya kutangaza nchi hiyo kwenye sekta mbalimbali zitakazosaidia kuvutia wawekezaji na kukuza uchumi wa taifa hilo ambalo ni miongoni mwa mataifa yaliyopiga hatua kubwa kiuchumi barani Afrika.



Mratibu wa Lishe na Jinsia kutoka Taasisi Kilele ya Kilimo cha Maua, Mboga, Matunda na Viungo (TAHA), Salome Stephen, akitoa elimu ya lishe kwa wananchi wa Kijiji cha Marito, Kata ya Shilela, Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mtalaam afya aeleza athari waliopata corona

Na Romana Mallya

MCHAMBUZI wa mambo ya afya, Dk. Elisha Osati, amesema baadhi ya watu waliougua ugonjwa wa corona na kupona wanarudi hospitalini wakiwa wamepata athari kwenye mapafu zinayosababisha kushindwa kupumua vizuri.

Katika mahojiano yake na redio Idhaa ya Kiswahili BBC yaliyofanyika juzi, Dk. Osati alisema wameanza kuona watu wanarudi wakiwa na athari hizo.

"Shida kubwa tunayoipata sasa hivi, wale wagonjwa waliopona corona, tumeanza kuona wanarudi wana athari, yaani mapafu yanapona kwa makovu sasa hawa watu wanapata shida sana ya kupumua na kufanya kazi zao.

"Hata ubora wa maisha yao yamekuwa chini kidogo na wanaendelea kutumia gharama kubwa sana kujitibu."

Dk. Osati ambaye pia ni Rais mstaafu wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), aliyasema hayo wakati alipoulizwa kuhusu chanjo ya corona na hatua zilizochukuliwa na Rais Samia Samia Suluhu Hassan, kukusudia kuunda kamati maalum kuchunguza ugonjwa huo ili kupata ushauri wa watalaamu hao.

Alisema hatua zilizokusudia kuchukuliwa dhidi ya corona imetoa faraja kwa sababu Tanzania inakwenda kufanya utafiti.

Jumanne ya wiki hii, Rais Samia, alisema anatarajia kuunda kamati maalum ya wataalam ya kuchunguza suala hilo na kuishauri serikali kwa kile alichosema Tanzania sio kisiwa, hivyo haiwezi kujitenga.

"Halifai kulinyamazia, ama kulikataa au kulikubali bila kufanya utafiti wa kitaalam, tutafanya utafiti wa kitaalam, tutaunda watalaam, watuambie upeo wa swali au tatizo hili lilivyo na hayo yanayopendekezwa na ulimwengu kuja kwetu, je, yakoje kitaalam, kwa utaalam wetu wa ndani," Rais Samia alisema.

Kauli hiyo ya Rais Samia aliitoa wakati wa hafla ya kuwaapisha makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu na wakuu wa taasisi na idara za serikali aliowateua Jumapili, wiki iliyopita. Dk. Osati alisema wanaamini timu hiyo itakwenda kushauri mambo makubwa matatu.

"Kuweza kuzifanyia utafiti mzuri wa kisayansi ambayo itatoa matokeo mazuri ikiwa dawa hizo zimesaidia kwa kiasi gani au hazijatusaidia, kuchukua tahadhari kwa ujumla kwa sababu tunaamini ukishatoa taarifa na watu wakaelewa watachukua tahadhari kubwa kama tulizochukua mwaka jana."

**CHANJO**

Dk. Osati alisema kamati hiyo inatakiwa kushauri kuhusu suala la chanjo kwa sababu katika hali ya sasa hawawezi kuikimbia.

"Kama alivyosema mama hiki sio kisiwa, suala la chanjo hii kamati lazima iangalie zilizopo duniani ipi inafaa kwa Tanzania na kwa gharama gani na ipatikane wapi," alisema.

Akifafanua, alisema kuna jambo ambalo watu wanapaswa kuelewa kwamba lengo kubwa la chanjo ambazo zimekuja sio kuzuia mtu kutopata corona bali zinazuia mgonjwa asipate ugonjwa mkali.

"Ukipata ugonjwa mkali maana yake unaweza kulazwa, unaweza kwenda ICU (Chumba cha Uangalizi Maalum) ukapewa mashine ya kusaidia kupumua au ukafa."

"Lakini, hata ukipona unaweza kuwa na madhara mengine, kuna kitu tunaita madhara baada ya corona ambayo ndiyo tunayaona sasa.

"Kumekuwa na propaganda nyingi kuhusu chanjo, ambayo kamati hii inatakiwa ikae kuangalia na kutueletea ukweli ni upi, chanjo hizi kwa mfano zipo zinazoweza kukukinga mpaka asilimia 95 mtu asipate ugonjwa mkali na nyingine zinaweza kuzuia hadi asilimia 100 mtu asipate ugonjwa mkali, ambazo ndiyo lengo la hizi chanjo," alisema.

Mtaalam huyo alisema kamati hiyo anadhani itatumia maabara za Tanzania na wataalam wake ambao watachambua kuona chanjo ipi inafaa kutumika.

Kuhusu tamko la Rais Samia, alisema lina maana kubwa kwa Watanzania kwa sababu ni ukweli karibu kila familia imeguswa na mgonjwa wa corona.

Alisema kwa hatua zinazochukuliwa sasa sio muda wa kulaumu kama Tanzania imechelewa au imewahi, kwa sababu hakuna mtu ambaye amewahi kufanya uamuzi sahihi. "Ndio maana katika nchi ambazo zimewafungia watu wake ndani bado ugonjwa unaendelea kuwapo, ndio maana ninasema hii kamati siyo wakati wa kulaumiana, wakae wafanye kazi ya kisayansi watuletee majibu.

# CAG: Mapato ya bil. 18.8/- ya h'shauri hayakupokelewa benki

Na Romana Mallya

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), imebainisha mapato ya Sh. Bilioni 18.8 zilizokusanywa na halmashauri 135 na hayakupelekwa benki.

Katika taarifa yake, CAG, Charles Kichere, alisema alipitia taarifa za makusanyo ya mamlaka za serikali za mitaa 135 na kubaini kuwa Sh. bilioni 18.8 zilikusanywa kutoka vyanzo mbalimbali, hata hivyo hakuna ushahidi unaoonyesha kiasi hicho kiliwasilishwa benki.

"Hii inaashiria usimamizi hafifu wa mapato. Kutopatikana kwa nyaraka zinazoonyesha mapato yaliyokusanywa yalipelekwa benki kulinizuia kujiridhisha kuhusu uhalali, usahihi na ukamilifu wa kiasi cha mapato kilichokusanywa na kuwekwa kwenye taarifa za fedha za halmashauri husika," alisema.

Alisema mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo huo ni Sh. bilioni 1.337.

"Nilipitia taarifa mbalimbali za ukusanyaji wa mapato katika halmashauri 22 na kubaini kiasi cha Sh. bilioni 1.34 kilikusanywa kwenye leseni za biashara na vyanzo vinginevyo nje ya mfumo wa mapato," alisema.

Kichere alisema mapato yanayokusanywa nje ya mfumo yanaweza kutumiwa vibaya na wakusanyaji bila kugundulika kwa kuwa hayaonekani kwenye humo hivyo kutoa mianya ya upotevu wa mapato.

"Miamala ya Sh. bilioni 4.792 iliyofutwa kwenye mfumo wa mapato bila kuwa na viambatisho muhimu, nilipitia marekebisho ya miamala kwenye mfumo wa mapato katika halmashauri 35 na kubaini kuwa kiasi cha Sh. 4,792,502,078 kilifutwa kwenye mfumo bila kuambatanishwa nyaraka muhimu za marekebisho hayo.

"Na wakati mwingine marekebisho hayo hayakuidhinishwa na Mweka Hazina au Ofisa Masuuli, kinyume na agizo la 37(6) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009," alisema.

Alisema miamala iliyofutwa kwenye mfumo wa mapato bila kuwa na viambatisho muhimu inaongeza hatari ya kutumika vibaya kwa mapato ya mamlaka za Serikali za Mitaa.

Alisema mapato ambayo hayakukusanywa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ni Sh. bilioni 30.86.

"Nilipitia taarifa mbalimbali za mapato zinazotokana na Mfumo wa Mapato (LGRCIS) na kubaini kuwa Sh. bilioni 30.86 hazikukusanywa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa 124 kutokana na mauzo ya viwanja, ukodishaji wa vibanda, leseni za vileo na vyanzo vingine.

Alisema hali hiyo inaonyesha kuwa Halmashauri hazikuwa na ufanisi wa ukusanyaji mapato.

Alisema mapato ya Sh.179,539,936 yaliyokusanywa, yalitumika kabla ya kupelekwa benki.

## Ndugai afichua siri hati chafu

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema hoja za ukaguzi zilizobainishwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kwenye halmashauri zinasababishwa na kuwapo na wahasibu wabovu.

Akizungumza baada ya Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Yusuph Masauni, kujibu swali la Mbunge wa Kibamba (CCM), Issa Mtemvu, Spika Ndugai alisema katika taarifa ya CAG matatizo yaliyojitokeza yamesababishwa na wahasibu.

"Ukiziangalia unaziona baadhi ya halmashauri matatizo yaliyojitokeza yamesababishwa na wahasibu wana uhasibu mbovu wengine wamefanya hivyo, halmashauri zingine wakahamishiwa zingine na kila anapohamishiwa anasababisha hati chafu na za mashaka eti vocha hazionekani nani anahifadhi kama si mhasibu?" alihoji.

Kutokana na tatizo hilo, Ndugai alishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuangalia suala la wahasibu wa aina hiyo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua ni lini serikali itatekeleza kikamilifu waraka namba tatu wa mwaka 2015 kuhusu muundo wa kada ya uhasibu na ukaguzi wa ndani.

"Je, ni lini kitengo cha uhasibu na fedha katika wizara na sekretarieti za mikoa zitapewa hadhi ya kuwa idara," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Masauni alisema waraka huo ulianza kutekelezwa mnamo mwezi Julai, 2018 kwa kutenganisha kada ya maofisa hesabu na wahasibu.

"Kwa mujibu wa muundo huo mpya Wahasibu ni wale wenye CPA na wale wasio na CPA wanatambulika kama maofisa hesabu," alisema.

Aidha, alisema kuhusu kupandisha hadhi vitengo vya uhasibu na fedha katika wizara na sekretarieti za mikoa kuwa idara katika kuandaa miundo ya taasisi, vigezo kadhaa hutumika ili kufikia maamuzi ya kuwa idara, vitengo na sehemu.

"Kwa kuwa miundo hii hufanyiwa marekebisho mara kwa mara kwa kushirikiana na wataalamu wa miundo kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kujadiliwa katika ngazi ya uamuzi. Ni mategemeo yetu kwamba serikali itakapoona kuwa kitengo cha uhasibu na fedha kinakidhi vigezo kuwa idara, kitapewa hadhi hiyo," alisema.

# Serikali yasema vigumu kubadilisha faini makosa ya usalama barabarani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imesema haioni haja ya kubadilisha faini ya makosa ya barabarani kwa kuwa zimewekwa kwa ajili ya kupunguza ajali za barabarani na si kukomoa madereva.

Naibu Waziri wa mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Musoma Mjini (CCM), Vedasto Manyinyi.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itabadili faini za makosa ya barabarani ili kutofautisha adhabu ya bodaboda na magari.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema licha ya faini kutozwa Sh.30,000 kwa kosa lakini bado matukio ya ajali za bodaboda yanaongezeka.

Hata hivyo, alisema jeshi la polisi limepewa mamlaka ya kupiga mnada pikipiki itakayokaa kwa zaidi ya miezi sita kwenye kituo cha polisi na kwamba zilizopo bado muda haujafika wa kupigwa mnada.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alisema jeshi hilo linashikilia pikipiki nyingi katika vituo vya polisi kwa muda mrefu.

"Je, serikali haioni fedha nyingi zinapotea kwa pikipiki nyingi kuchakaa zikiwa katika vituo vya polisi, hivyo kuleta hasara kwa taifa?" alihoji.

Pia alihoji kwa nini serikali isiunde kamati maalum kila baada ya miaka mitatu kupitia sababu zilizofanya pikipiki hizo zishikiliwe kwa muda mrefu.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri alisema pikipiki ni chombo cha moto kinachotumika kufanya biashara ikiwamo kusafirisha watu kutoka sehemu moja kwenda nyigine na zipo sababu tatu zinazofanya kushikiliwa kwenye vituo vya polisi.

"Kundi la kwanza ni zile pikipiki zilizokamatwa kwenye makosa ya jinai ambazo zimetumika kutenda makosa au zilizoibwa toka kwa watu," alisema huku akibainisha kuwa kundi la pili ni pikipiki zilizokamatwa baada ya kutenda makosa ya usalama barabarani.

"Kundi la tatu ni zile pikipiki zilizookotwa na hazina wenyewe na kuhifadhiwa kituoni, hivyo pikipiki hizi ziko vituoni kama vielelezo vya kesi na vielelezo ambavyo havina mwenyewe na kuwapo kwake kituoni ni kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo," alisema.

Aidha, alisema serikali itaendelea kufuatilia kwa ukaribu mashauri yote yaliyopo Mahakamani yanayohusu vielelezo vilivyopo vituo vya Polisi yanamalizika kwa wakati ili mashauri hayo yasikae muda mrefu.

Aidha, alisema pikipiki na vyombo vingine vya moto kuondolewa kwake vituoni kunategemea na amri ya mahakama na uamuzi wa kesi.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene akijibu maswali ya wabunge bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Barabara ya Kolandoto – Kishapu yakumbukwa

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, asema barabara ya Kolandoto hadi Kishapu mkoani Shinyanga iko katika mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami kuanzia Juni, mwaka huu.

Kasekenya alisema hayo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kishapu, Nyangindu Butondo (CCM), aliyetaka kujua mpango wa serikali katika kuijenga barabara hiyo kutokana na umuhimu wake kiuchumi.

Mbunge huyo alisema barabara hiyo ina umuhimu wa kipekee kiuchumi na kwamba ni tegemeo kwa wananchi kusafirisha mazao yao ikiwamo pamba.

"Barabara hiyo ni barabara kuu na serikali inatambua umuhimu wake na ni kipaumbele cha serikali kuhakikisha barabara zote kuu zinakuwa kwa kiwango cha lami.

"Barabara hii iko kwenye mpango naamini kabla ya Juni, mwaka huu, tutakuwa tumeanza utekelezaji. Naamini katika mipango yetu, barabara hii itaendelea kutengewa fedha ili ikamilike," alisema.

Awali, alisema Wizara hiyo tayari imeanza maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara na kutenga Sh. bilioni 2.5 katika mwaka wa fedha 2020/21.

Kasekenya alisema barabara hiyo inayojulikana kwa jina la Kolandoto – Mwangongo yenye urefu wa kilometa 53 ni sehemu ya barabara ya Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Sibiti – Oldean B Junction Arusha, yenye urefu wa kilometa 328 inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

"Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii ili kuijenga kwa kiwango cha lami imekamilika, kazi hii ilifanywa na Mhandisi Mshauri M/S. Intercontinental Consultants and Technocrats Pyt Ltd ya India," alisema.

Aidha, alisema wakati maandalizi ya kuanza ujenzi yakiendelea, Serikali kupitia Tanroads inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hiyo ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka.

"Katika mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya Sh. milioni 443.31 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali," alisema.

Katika swali lake la msingi, Butondo ameitaka serikali kuharakisha ujenzi wa barabara ya Kolandoto hadi Kishapu kwa kiwango cha lami ambayo inaunganisha mikoa minne kiuchumi.

Alisema ni wakati wa serikali kuona umuhimu wa kujenga barabara hiyo ambayo wananchi wa Kishapu wanaitegemea kusafirisha mazao yao ikiwamo pamba.

Mbunge huyo alisema barabara hiyo imekuwapo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020, lakini haikutekelezwa kwa kipindi hicho.

"Pamoja na ilani ya uchaguzi kuainisha barabara hii itaenda kutekelezwa katika mpango wa mwaka 2020-2025? je, serikali haioni umuhimu sasa wa kuanza kujenga barabara hii?" alihoji.

Alisema barabara hiyo ni kuu na itaunganisha mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Singida na Arusha na kuitaka serikali itoe tamko la ujenzi wake ili kuchochea maendeleo kwenye maeneo hayo.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA



Ukurasa 13

Samia chungulia matobo zaidi uyazibe



Ukurasa 12

Ijue UTT, mfuko unaosajili tafsiri kuu ya uchumi binafsi na uwekezaji kimkakati

BUFE

IJUMAA APRILI 9, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

Corona inavyowadororesha wafanyabiashara wa bidhaa kutoka ukanda wa ughaibuni

# Wakulima korosho, ushirika wao Liwale wajipanga baada kombora

- Mrajisi Ushirika: Ndio kilimo kilivyo!
- Mwenyekiti Ushirika aanika mikakati

**Sabato Kasika,** LIWALE

KWA misimu miwili mfululizo uzalishaji wa korosho mkoani Lindi umeshuka kwa kiwango kikubwa na kusababisha wakulima kuanguka kiuchumi.

Taarifa ya Chama cha Ushirika cha Msingi Umoja (AMCOS) cha mjini Liwale pekee, katika misimu wa kilimo mwaka 2019/2020 na 2020/2021, makusanyo ya korosho yameshuka kutoka tani 3300, hadi tani 1700.

"Misimu ya nyuma hali ya uzalishaji ilikuwa nzuri na makusanyo yetu yalikuwa ni kati ya tani 3800 hadi tani 4500, lakini misimu ya mwaka juzi na mwaka jana hali imekuwa mbaya," anasema Mwenyekiti wa chama hicho aliyemaliza muda wake, Hassan Mpako.

Anafafanua, kwamba kushuka huko uzalishaji, kumewafanya wakulima kushindwa kumudu ununuzi wa pembejeo, kuwasomesha watoto wao na mahitaji mengine kama chakula na mavazi.

Mwenyekiti hiyo anataja sababu kubwa ya kuanguka kwa uzalishaji wa zao hilo ni kusuasua kwa soko, mashamba mengi kuwa na mikorosho ya zamani na kuchelewa kwa pembejeo muhimu, ikiwamo ya upulizaji dawa ya salfa.

Mpako anashauri umoja wao kuwa na makini, pia mikakati madhubuti, vinginevyo wakulima wataanguka kiuchumi, hivyo anasema uongozi wake uliomaliza hivi karibuni iliyopita, umeacha mapendekezo matano ya kujadiliwa kwa kina ili kuhakikisha uzalishaji korosho unaongezeka msimu ujao.



Mwenyekiti wa Umoja Amcos aliyemaliza muda wake, Hassan Mpako, akisoma taarifa ya hali ya uzalishaji wa korosho kwa msimu uliopita. **PICHA: SABATO KASIKA**

### MIKAKATI IPI?

Mkakati waliojiwekea anasema ni kuandaa mashamba mapya ambayo yatapandwa mbegu za kisasa kulingana na ushauri kutoka kwa wataalamu wa kilimo.

Pia, anasema wamependekeza kupitia na kuchambua orodha ya wanachama wasiozalisha na kuuza kwenye chama hicho, sambamba na haja ya kuhakikisha mikopo ya pembejeo inapatikana kwa masharti nafuu, ili kumuwezesha mkulima amudu kuhudumia mashamba yake na uzalishaji uongezeke.

"Kutoa elimu ya matumizi bora ya pembejeo kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu ili kuwawezesha wakulima na wanachama kuhudumia mashamba yao kwa gharama nafuu na kuepuka hasara zinazoweza kuzuilika," anasema.

Anautaja mkakati mwingine, ni kuimarisha uwajibikaji na weledi katika usimamizi na utendaji wa viongozi mbalimbali.

Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Lindi, Edmund Massawe, anawataka wakulima wa korosho kutokata tamaa baada ya kushuka uzalishaji, bali iwe fursa ya kujipanga kwa ajili ya msimu ujao.

Anawaomba wakulima 'wasitafute mchawi', bali watambue kilimo kina matatizo, baadhi yakiwa ndani ya uwezo wao kuyatatua. Massawe anaendelea: "Kushuka kwa uzalishaji wa korosho katika msimu uliopita, muichukulie kama fursa, mkae mtafakari kwa kina kisha mjipange upya kwa ajili ya msimu ujao."

Mkulima kutoka chama hicho, Mohamed Mnoche, anasema msimu uliopita walijitahidi, lakini matokeo hayakuwa mazuri. Anasema: "Wakulima wenzangu tusikate tamaa, tusonge mbele ipo siku tutavuna korosho za kutosha kama ilivyokuwa miaka ya nyuma na inawezekana msimu ujao ukawa wetu, tumuombe Mungu."

### MIAKA YA MAFANIKIO

Mpako anaorodhesha hatua za mafanikio walioanza nayo katika chama kabla ya kusuasua katika misimu iliyopita ni kubuni vyanzo vipya vya mapato; kununua mashine ya kukamua mafuta ya alizeti, kujenga vibanda vya biashara, kujenga ghala la kuhifadhi mazao na kununua mzani mkubwa.

Anakumbusha hatua ya kwanza miaka sita iliyopita, alikuwa na wanachama 478, lakini hadi sasa wapo 1045, Mpako akijinadi:

"Kwa wale wasiojua ni kwamba, umoja ulikuwa na ghala moja lenye uwezo wa kuchukua tani 5,000, lakini tumeongeza lingine lenye uwezo wa kuchukua tani 8,000 hadi 10,000 kwa mkopo wa benki ya NMB."

Kwa mujibu wa Mpako umoja huo ulishakopa benki Sh. milioni 500 za ujenzi wa ghala hilo, huku Sh. milioni 100 nyingine zikiwa zimetolewa na umoja wao kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa ghala hilo ambalo sasa linafanya kazi.

Pia, anataja kingine cha kijamii kilichochangiwa na umoja huo, ni kujihusisha na maendeleo ya jamii, kwa kuchangia ujenzi wa shule na kununua magodoro 50 kwa ajili ya Shule ya Sekondari Makata.

UCHUMI

# Ijue UTT, mfuko unaosajili tafsiri kuu ya uchumi binafsi na uwekezaji kimkakati

- ‘Waliobipu’ waeleza mitaji yao ‘iliyoitika’

**Na Frank Monyo**

KATIKA miaka ya hivi karibuni kumekuwapo mwamko wa Watanzania kujikita katika uwekezaji wa aina tofauti, kwenye kampuni zinazojihusisha na masula hayo.

Kampuni ya UTT AMIS iliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, imekuwa na mchango mkubwa kwa wananchi na taasisi za kimataifa katika kuchochea, maendeleo ya uchumi kijamii na kitaifa kwa ujumla.

Ni miaka 10 sasa UTT AMIS inasimamiwa na Wizara ya Fedha, ikitoa fursa kwa Watanzania wenye vipato vya aina zote na nyadhifa tofauti kuwekeza kwa manufaa yao, watoto na taifa kwa ujumla.

Ofisa Mwandamizi wa Masoko na Uhusiano wa UTT AMIS, Rahim Mwanga, anasema taasisi hiyo ina jukumu la kuanzisha na kuendesha mifuko ya uwekezaji kwa mujibu wa Sheria ya Masoko, Mitaji na Dhamana nchini.

Mwanga anasema serikali ilikuwa na lengo la kuleta wigo mpana kwa wananchi, kuwawezesha kuweka akiba na kuwekeza kupitia masoko ya fedha na mitaji, ili kushiriki katika kumiliki uchumi wa nchi kutokana na mabadiliko ya sera za uchumi katika nyakati hizo.

“Serikali ilitaka kuleta ushiriki mpana wa wananchi, kwenye uchumi kwani kulikuwa na sera ya ubinafsishaji wa kampuni ya serikali, kukawa na changamoto kubwa kwa Watanzania.

“Changamoto hiyo ilikuwa kwamba, je baada ya hatua hiyo na kufunguka kwa uchumi wa soko, huyu mwananchi wa Tanzania anapata manufaa gani na uwapo wa masoko ya fedha na mitaji?” anahoji Mwanga

### MIFUKO INAWAJIBIKAJE?

Ofisa huyo wa masoko wa UTT AMIS, imepewa leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), inayowawezesha kukusanya amana kutoka kwa wawekezaji na kuziwekeza.

“Tukishapata hizo fedha tunaenda kuwekeza katika mfuko husika kulingana na waraka wa toleo la mfuko. Mifuko yetu tuliyonayo inawekeza katika sehemu kubwa mbili ambazo ni masoko ya fedha na masoko ya mitaji.

“Faida inayopatikana inarejeshwa na kugawanywa kwa wawekezaji na sehemu ya uwekezaji wao katika mfuko ndio inafahamika kama kipande,” anafafanua Mwanga.

### FAIDA YA KUWEKEZA

“Faida katika uwekezaji huu wa pamoja ni mwekezaji kuwa na nafasi ya kupata faida shindani, ukilinganisha na bidhaa za uwekezaji wa namna hiyo katika soko, huku hatari za uwekezaji zikipunguzwa kwa kufanya uwekezaji mseto.

“Pia, mifuko ya uwekezaji inawezesha wawekezaji wadogo kupata fursa za kuwekeza kwenye masoko ya fedha na mitaji kwa viwango vidogo vya fedha, tena mara kwa mara.

“Wawekezaji, pia wanapata fursa ya kuwekeza kwenye dhamana ambazo katika hali fulani mwekezaji mmoja mmoja inakuwa ni ngumu au ghali kuweza kupata dhamana hizo,” anasema.



Wanachama wa UTT AMIS wakiwea kikaoni. **PICHA: MTANDAO**

> **Hivyo, pesa niliyoweka zaidi ya milioni tano ambayo nategemea kupata gawio baada ya mwaka na nitakuwa nimeongeza mtaji wangu katika biashara niliyotamani kuifanya.**



Ofisa Mwandamizi wa Masoko na Uhusiano wa UTT AMIS, Rahim Mwanga , akitoa elimu kwa wadau wa Unguja, katika eneo ka Kariakoo. **PICHA: FRANK MONYO**

### MNUFAIKA ANENA

Tausi Mwakasongo (43), ni mkazi wa Bagamoyo mkoani Pwani, anakiri uwekezaji alioufanya kununua vipande UTT AMIS umekuwa dira katika maisha yake.

Mjane mwenye watoto wawili, anasema baada ya kupata elimu juu ya uwekezaji kupitia mifuko hiyo na kumemfanya awe na shughuli zake za ufugaji, kwa mafanikio sambamba na kusomesha watoto wake bila wasiwasi wa kukwama ada.

“Nilikatishwa sana tamaa, waliamini sitaweza kuwasomesha watoto wangu nilioachiwa na marehemu mume wangu, lakini namshukuru Mungu kwa sasa mimi ni mwalimu wao katika mafanikio,” anasema

Anasimulia kuwa mwaka 2009 alianza kuwekeza na kununua vipande kwenye kiitwacho Mfuko wa Wekeza Maisha na Mfuko wa Watoto, lengo ni kuwekeza kwa manufaa ya elimu ya watoto na maisha yake kwa ujumla.

“Wakati naanza kuwekeza mwaka 2009, nilikuwa tayari na ng’ombe wawili niliokuwa nakamua lita 20 kwa siku. Nilikuwa nauza lita moja Sh. 1,500, biashara ikiwa nzuri kwa mwezi nilikuwa napata Sh. 900 ,000.

“Nikaona nianze kuwekeza katika mfuko wa Wekeza Maisha na Mfuko wa Watoto kupitia kipato hiki ninachopata ili kiweze kunisaidia mimi na watoto wangu baadae,” anasema.

Mfuko wa Wekeza Maisha, ni namna ya kuwekeza kwa muda wa miaka 10, ukiwa umeambatanishwa na faida za bima, mwekezaji wa mfuko huo anaweka lengo la kiasi anachotaka kuwekeza katika muda huo.

Inatajwa kiwango cha chini kikiwa ni Sh.milioni moja, mwekezaji anaweza kuwekeza kwa mkupuo au kwa awamu.

“Bima ambazo zinatolewa na mfuko ni bima ya maisha, ulemavu wa kudumu na bima ya ajali, hii ndio moja ya faida ya kuwekeza katika mfuko huu,” anasema.

“Baada ya miaka 10 niliweza kufungua kiwanda kidogo nyumbani kwangu cha kusindika maziwa na nilifanikiwa kuongeza ng’ombe saba majike na dume wa mbegu mmoja, kwa sasa kipato changu kimeongezeka sana,” anasema Tausi.

### MFUKO WA WATOTO

Anasema wakati mume wake anafariki, alimuachia watoto wawili wa kike akiwa na miaka miwili na wa kiume mwenye mwaka mmoja.

“Nilijiunga na Mfuko wa Watoto kwa ajili ya ada ya watoto wangu na mahitaji ya shule, kila mmoja nilimfungulia akaunti yake, hii ilinisaidia sana kwani kwa sasa mtoto wangu wa kwanza anaingia sekondari na uhakika wa elimu bora kwa mtoto wangu sina wasiwasi na suala la ada,” anasema na anaongeza:

“Mfuko wa watoto una lengo la kumpatia fursa mzazi kuanza kuwekeza mapema kwa ajili ya elimu ya Sekondari hadi Chuo Kikuu kwa ajili ya wanaye. Kiwango cha chini cha kuanza kuwekeza ni Sh. 10,000, na kiwango cha chini cha nyongeza ni shilingi 5, 000,” anasema.

### WANUFAIKA KIBIASHARA

Samia Ngonyani ni mfanyabiashara mwenye simulizi yake: “Nilikuwa na ndoto ya kufanya biashara ya kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi lakini baada ya kuibuka kwa janga la corona, mipaka ikafungwa na biashara zikasimama hasa China, kwa sababu ya ‘lock down’ (kufungiwa majumbani)

.“Ile pesa niliyotaka kuagizia mzigo ikanibidi niwekeze katika Mfuko wa Ukwasi (Liquid Fund) huku nikisubiri hali ikae sawa. Nilijiunga katika mfuko wa Kujikimu, ambao unatoa gawio mara kila mara, huku lengo lake kubwa likiwa kukuza mtaji kwa muwekezaji.

“Hivyo, pesa niliyoweka zaidi ya milioni tano ambayo nategemea kupata gawio baada ya mwaka na nitakuwa nimeongeza mtaji wangu katika biashara niliyotamani kuifanya,” anasema Nyamaka.

### MSTAAFU MNUFAIKA

Fabiani Nyato, ambaye ni mstaafu katika taasisi moja ya kiserikali ambayo hakutaka kuitaja jina lake, anasema kuwa UTT AMIS imemsaidia kutunza fedha zake za kiinua mgongo kwa faida huku akifanya utafiti afanye biashara gani.

Anasema kuwa kati ya fedha zake za kiinua mgongo alizolipwa aliamua kuwekeza katika mfuko wa Hatifungani(Bond Fund), ambao kwa Ofisa wa UTT, Mwanga, anasema mfuko huo una lengo la kutoa gawio kila mwezi na kila baada ya miezi sita huku pia kukiwa na mpango wa kukuza mtaji.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Samia chungulia matobo zaidi uyazibe






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

“TREND mnayokwenda nayo sasa hivi ni kuua walipa kodi, mnaua wafanyabiashara, mnatumia nguvu kuliko akili na maarifa kupata kodi, mnawakamua, kuchukua vifaa vyao vya kazi, mkafungia akaunti zao, mkachukua pesa kwa nguvu kwenye akaunti kisa sheria inakuruhusu ni mnapunguza walipa kodi!”

Hii ni kauli mujarabu kabisa kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyekula kiapo chake cha urais Machi 19, mwaka huu pale Magogoni Dar es Salaam, akichukua urithi kutoka kwa Dk. John Pombe Joseph Magufuli, aliyeaga dunia Machi 17, mwaka huu Dar na kuzikwa Machi 26 Chato.

Alitoa kauli hii Aprili Mosi, mwaka huu pale Chamwino, Dodoma, akiapisha viongozi aliowateua Machi 31. Waliomsikiliza baadhi hawakuamini, wakidhani pengine ni Siku ya Wajinga, lakini ndivyo mama huyu shupavu alivyomaanisha, akiendelea kujibainisha kuwa ni Rais katika maumbo ya mwanamke.

Alikuwa akituma ujumbe kwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, akimtaka yeye na wenzake kutumia busara zaidi katika kukusanya kodi, badala ya kutumia misuli ya kifua, mikono na miguu na kusababisha wafanyabiashara kujiona wanaporwa na kufunga biashara zao na wengine kukimbia.

Sijui ni kwanini mpaka RaisSamia afike huko? Hivi kwa akili za kawaida tu, watu hawakujua kuwa huwezi kutumia nguvu kumkamua ng’ombe ambaye anaweza kukutwisha teke, ukagalagala huko chali?

Kwani ugumu ulikuwa wapi kukaa na wafanyabiashara chini na kujadiliana jinsi ya kugawana faida na kila mmoja asiumie? Kwani unapomdai mtu, ni mpaka umwendee na mapanga hata kabla hujazungumza naye? Midomo na ndimi Mungu aliviumbia nini kwa binadamu? Kula tu!!

Mfanyabiashara ameajiri watu 5,000 mathalani nchini, ana vitega uchumi kibao, kila kona ya nchi nna kote huko kuna wafanyakazi. Anafuatiliwa pengine hata kwa sababu binafsi tu, anasingiziwa hiki na kile, pengine anafikishwa kortini bila ushahidi, anachomoka anatafutiwa lingine.

Anabambikiwa kesi ya kukwepa kodi, anakamatiwa akaunti zake, anafungiwa biashara zake, hatimaye anaona isiwe tabu anatimka anakwenda kufanya biashara zake zingine Ughaibuni. Huku nyuma wale wafanyakazi wake wenye kila mmoja familia ya watu sita, wanafanyaje?

Ukidhani umemkomoa, kumbe umekomoa Watanzania wenzako waliokuwa wakitegemea mkate kuletwa na mwajiriwa wa mfanyabiashara huyo. Ukidhani umemkomoa, kumbe umekomoa nchi yako iliyokuwa inakusanya kodi kutoka kampuni na viwanda vyake.

Unakaa unakodoa macho, miradi inakushinda, unalalamikia vifanyabiashara vidogo vidogo vikiwamo vimachinga eti vinakwepa kodi, huku wakubwa umeshawachanganya wamehamishia mitaji kwa jirani na Ughaibuni. Umepata nini? Aibu tu kwa watu wako.

Hicho ndicho RaisSamia alichokiona na kukikataa kuanzia mwanzo na tunadhani atakwenda mbali zaidi kuona, ni kwa namna gani hali ya hewa kwa wafanyabiashara inawaruhusu kuendelea kuwapo na kulipa kodi salama, pia kuvuta wengine kuja kuwekeza.

Rais Samia amejua wazi kuwa kuna watu hutengeneza fitina na chuki zao dhidi ya wafanyabiashara kwa ugomvi wao pengine wa utotoni, ukubwani au ulevini na kukomoana kwa sababu mmoja kashika mpini, mwingine makali.

Alivyoanza na anavyoenenda Rais Samia, ni dhahiri kuwa siku moja atesema, “wale mliokimbia nchi kwa sababu moja au nyingine inayoshabihiana na mchafuko wa hewa uliosababishwa na watu, basi rudini nchini muendelee kuijenga nchi yenu.”

Si ajabu wapo hata walio wazawa wa nchi, wako tayari kufia kwao wakifanya shughuli zao kama ilivyokuwa zamani, wako tayari kusamehe mitama waliyopigwa na kudondoka na sasa kuendelea na Tanzania yao njema. Hongera Rais Samia, endelea kuchungulia matobo uyazibe. Alamsiki!

BIASHARA

# Corona yageuka shubiri kwa waagizaji bidhaa kutoka ukanda wa ughaibuni

Na Jenifer Gilla

UGONJWA wa mlipuko duniani, Corona, umeleta changamoto kadhaa katika sekta ya biashara nchini, mojawapo ni kuwakwaza wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa nje ya nchi.

"Nilipokea mzigo ukiwa na viatu 200 vyenye ubora wa chini tofauti na hela niliyolipia ni sawa na ulipie Sh.15000 wa kupe kiatu cha Sh.5000. Ilikuwa ni hasara kubwa kwangu, nilichanganyikiwa, nilipata hasara ya karibu milioni tatu".

Huyo ni Bertha Mmari (35), mkazi wa Kimara, Dar es Salaam, mfanyabiashara wa jumla wa nguo na viatu, anataja moja ya hasara anazozipata kutokana na kuagiza mzigo kwa njia ya mtandao kutoka nchini China.

Awali, Bertha anasema akisafiri mpaka nchini China na kuchagua bidhaa kuzifunga kwenye maboksi, kisha akazipeleka sehemu ya kusafirisha mizigo kuja nchini Tanzania.

Mfanyabiashara huyo anaeleza kuzuizi kinachomsitisha kwenda China kufuata mzigo, ni mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona, inayoendelea kuitesa nchi hiyo, pia kwingineko duniani, hata kuwazuia kutoka mataifa mengine kuingia humo kwa sasa.

Pia, Bertha, anaeleza usalama mdogo wa mizigo yao sasa, mingi ikiibiwa na wafunga mizigo, katika sehemu za usafirishaji.

"Ukiwapo wakati wanafunga kwenye maboksi kuipeleka kwa wakala, ni tofauti na ukimuagiza wakala akufungie. Hivyo, ikifika kwenye mikono ya wasio waaminifu wanakuibia au kukubadilishia mzigo," anasema.

Malalamiko mengine ya wafanyabiashara, ni ni suala la mizigo kuchelewa, tangu mara ilipozuka maradhi ya corona.

Roda Mwakanele (39) Mfanyabiashara wa nguo za kike eneo la Sinza, Dar es Salaam, anayesimulia: "Niliagiza mzigo tangu Oktoba mwaka jana nikilenga niuze kipindi cha msimu wa sikukuu, lakini mzigo umefika mwezi huu wa kwanza ambapo hakuna biashara kabisa."

Kwa ujumla, kuna majumuisho kwamba, kama ilivyokwa usafirishaji, hata kasi ya uzalishaji viwandani imezorota nchini China.

Mama huyo mfanyabiashara anatoa ushuhuda kwamba, awali oda ya bidhaa ilichukua wiki moja hadi mbili kutengenezewa aina ya nguo mtu atakayo, sasa inachukua kai ya mwezi hadi mwezi na nusu.

Frida Mmari (45), ni mfanyabiashara hao anayelalamika kutopokea mzigo aliyouagiza tangu Oktoba mwaka jana, akilenga kipindi cha sikukuu.



Mandhari ilivyo maduka ya jumla nchini China. **PICHA: MTANDAO**

"Nilitegemea kuuza mzigo huo wa nguo za watoto kipindi cha sikukuu (Krismasi), lakini mpaka leo sijapokea.

"Nipo tu sasa sielewi nifanyeje, na siwezi kuagiza mwingine hadi huo ufike, haya mambo kabla ya Corona hayakuwapo," analalamika Frida.

Licha ya changamoto wanayoipitia wafanyabiashara hao hawatasita kusifia faida inayopatikana kutokana na kuagiza kwa njia ya mtandao. Bertha anasema, mtu akiagiza mzigo kutoka nje ya nchi unaokoa nauli ambayo ni zaidi ya Sh. milioni mbili, kujumuisha na pamoja na hela ya chakula na malazi kwa siku utakazokaa huko.

"Ukienda mwenyewe kuna gharama kubwa unaweza kutumia hata shilingi milioni 2 za Kitanzania kwa wiki mbili tu utakazokaa, lakini ukiagiza mwenyewe 'unasave'(kukoa), pesa nyingi" anasema.

Rhoda Mwakanele naye anakiri, mfanyabiashara anayefuata mzigo China, anatumia muda mrefu na duka lake linakosa mtu wa kulisimamia kwa usahihi hata kuishia hasara.

Pamoja na kuwapo changamoto hizo, wafanyabiashara hao hawajakata tamaa, wanaendelea na uagizaji bidhaa China.

"Uvumilivu ndio nguzo kuu katika hali tuliokuwa nayo kwa sasa. Pia, kama unajiweza agiza mzigo mkubwa ambao utakaa nao muda mrefu, kwa sababu kwa hali ilivyo sasa hakuna tutakachoweza kufanya zaidi ya kusubiri" anasema Rhoda

### WASAFIRISHAJI WATETA

Ofisa wa Huduma kwa Wateja kutoka kampuni ya usafirishaji mizigo ya Choice Shipping Tanzania, Nuru Ezekiel, anaeleza malalamiko ya mizigo kuchelewa kufika hasa kwa wateja wenye mizigo midogo hutokana na meli kuwa chache, baadhi yao zikiwa zimesitisha huduma ya usafirishaji.

Nuru anasema, hata katika ofisi zao zilizopo China ambako ndipo mizigo inapakiwa nguvu kazi imepungua kutokana na wafanyakazi kurejea nchini kupisha maambukizi ya corona.

Pia viwanda vingi nchini China vimefungwa na vilivyopo vichache vinaelemewa na oda, akitoa mfano wa kazi ambayo zamani ilichukua siku tatu hadi wiki moja, hivi sasa ni wiki mbili na zaidi.

Kuhusu ya walakini katika oda na mzigo inayoletwa, Nuru anaeleza: "Hilo la kuibiwa na kudhulumiwa sisi hatuhusiki. Sisi tunakwenda kuchukua mzigo, wengine tunakuta wameshaufunga tunabeba boksi tunaondoka, hayo mengine hatujui."

> **"Kwa utapeli unaohusisha nchi za nje tunafuata utaratibu za kisheria kwa nchi hizo mbili hapo tukihusisha pia na Shirika la Polisi wa Kimataifa, Interpol.**

Kibiashara analalamika kupata hasara, kutokana na changamoto hiyo ya usafiri na kwa sasa wanapoteza wateja, wengi wanakimbilia kwingineko, wakidhani kuna unafuu

"Wateja wengi tunaona wanahama, wakidhani kuwa huko waendako kuna nafuu, lakini wengine wanarudi baada ya kuona kuwa kumbe changamoto zinafanana," anasema

Ofisa huyo aneleza uamuzi waliochukua kukabili hilo, wamesitisha usafirishaji mizigo kwa kutumia meli, sasa wanatumia ndege mpaka hali itakapokaa sawa, ingawa gharama zake zipo juu kulinganisha na meli.

### TCRA WANENA

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma wa Mamlaka ya Mawasiliano Nchini (TCRA), Semu Mwakyanjala, alisema kuwa wanapokea kesi kama hizo za ndani na nje ya nchi na wanatoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi ili kupatikana kwa wahalifu ili kukamilisha uchunguzi.

"Kwa utapeli unaohusisha nchi za nje tunafuata utaratibu za kisheria kwa nchi hizo mbili hapo tukihusisha pia na Shirika la Polisi wa Kimataifa, Interpol", anasema.

Hata hivyo Mwakyanjala anawasihi wafanyabiashara wanaonunua bidhaa mtandaoni kuwa makini kwa kufanya uchunguzi kabla ya kuagiza bidhaa.

"'Sasa hivi mawasiliano yamerahisishwa, watu wanaweza kununua na kuuza bidhaa mtandaoni lakini pia kuna watu wanaotumia mitandao vibaya kutapeli wengine hivyo anawasihi Watanzania kuwa makini.

Hasa hawa wanaoagiza nje ya nchi inabidi wafanye utafiti na kujiridhisha kabla hawajaagiza bidhaa kwa mtu na kumtumia pesa nyingi, "anamalizia.

Akizungumzana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya miundombinu hivi karibuni, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile anasema takriban kuna miamala milioni 300 inafanyika, serikali ikipata Sh. bilioni 80 za tozo.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia, nchini Tanzania kuna asilimia 40 ya wanawake nchini wanajishughulisha na biashara.

Pia, hadi kufikia Aprili 7, mwaka huu, Shirika la Afya Duniani (WHO) linaripoti kuna maambukizi 132,046,206 ya ugonjwa wa Corona na vifo 2,867,242 ulimwenguni.





# Waahidi kuendelea kumuenzi Magufuli

**Na Peter Mkwavila,** MPWAPWA

BAADA ya taifa kumaliza siku 21 za maombolezo ya Hayati Rais John Magufuli, wananchi wa Kata ya Lufu na Galigali Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, wamesema wataendelea kumuenzi kutokana na kuwawesha kufikiwa na miundombinu mbalimbali ya kimaendeleo.

Diwani wa kata hiyo, Lelisi Mwachali, alisema tangu Tanganyika ilipopata uhuru mwaka 1961, kata hizo na vijiji vyake hazikuwahi kuwa na barabara za kupitika kwa pikipiki baiskeli wala gari, wananchi wake ilikuwa inawalazimu kutumia punda na kutembea mwendo mrefu zaidi ya masaa nane kuelekea vijiji vya jirani kutafuta mahitaji.

Alisema kuwa kabla ya utawala wake na kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), wagonjwa wakiwamo kinamama, watoto na wazee walikuwa wanabebwa kwenye vitanda kutafuta huduma za kujifungua.

Alisema baada ya kuingia madarakani Rais Magufuli vijiji vingi vya wilaya hiyo ya Mpwapwa vilianza kutegenezwa na wananchi wakapata uhuru wa kuwa na barabara zinazopitika kwa wakati na hata vyombo vya usafiri vikawa vingi.

Arnord Mwakitinya alisema miongoni mwa kata zinazojishughulisha na kilimo cha mboga, mahindi, na uwele ambapo hapo awali walikuwa wanashidwa kunufaika kutokana na barabara hizo hivi sasa kupitika kuingia na kununua mazao hayo .

Maria Lawlence, mkazi wa Lufu, alisema kuwa kabla barabara hizo kujengwa kinamama wengi walipoteza maisha wakati wa kujifungua na wengine walikuwa wakizalia maporini. Maria alioimba serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kuwaboreshea huduma za jamii ikiwamo za kiafya na masoko ya mazao yao, kwa kuwa walio wengi wanauza kwa walanguzi ambao huwalalia bei na kutonufaika na kilimo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, alisema kuwa walipokea fedha za ukarabati barabara ya Kibakwe, Mwanawota, Lwanda Galigali na Kidenge Lufu ambazo zilifanya mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii katika kata hizo.

Shekimweri alisema kuwa pamoja barabara, miundombinu mingine kwa wananchi wa wilaya hiyo pia kuna vitu vingi vya kumkumbuka Hayati ,Magufuli kwa sekta ya elimu, afya na miundombinu..

Alisema serikali chini ya Dk. Magufuli iliweza kutoa zaidi ya Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo ikiwa na lengo la kufungua fursa za kata hizi kiuchumi, kielimu na huduma za jamii.

Alisema kukamilika kwa barabara hizo kulifungua fursa nyingi katika kata husika ikiwemo kuboreka kwa huduma za jamii, pamoja na kukuza uchumi kwa maeneo mbalimbali kwa kusafirisha mazao yao kirahisi na wanunuzi kufuata bidhaa hadi vijijini.

# Lukuvi aombwa kibali cha ujenzi Chang'ombe

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKAZI wa Mtaa wa Mtakuja mji Mwema Kata ya Chang'ombe jiji la Dodoma, amemuomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wiliam Lukuvi, kutoa kibali cha ujenzi wa nyumba kwenye maeneo yao ili kuondokana na maisha duni ya kukosa makazi bora.

Ombi hilo kwa Waziri lilitolewa na wakazi hao kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Mji Mwema, ambao ulikuwa maalumu kwa ajili ya kumuomba waziri huyo ili aweze kutoa kibali kitakachowawezesha kujenga makazi bora tofauti na wanavyoishi hivi sasa.

Waziri Lukuvi alisimamisha ujenzi wa nyumba kwenye mtaa huo Julai15, 2020, kwa madai kuwa kampuni iliyopima ya J.F. kwenye mtaa huo ilikuwa haitambuliwi kisheria na serikali na imefutwa.

Wakizungumza kwenye mkutano huo, wakazi hao Daniel Kiula, alisema kuwa toka walivyosimamishwa kuendeleza maeneo yao, maisha yao yamekuwa ni duni kwa kuwa walio wengi pamoja na kuwa wana hati lakini wanashindwa kokopea fedha ili waweze kujenga nyumba za kisasa.

Pili Sukuma, alisema wanamuomba waziri huyo mwenye dhamana kuwatatulia changamoto hiyo iliyojitokeza ya kuzuiliwa kujenga nyumba kwenye maeneo hayo, ili aweze kutoa kibali ambacho yeye aliamuru kuisimamisha kampuni hiyo ilikuwa ikipima na ambayo ilidaiwa kuwa haitambuliwi kisheria na serikali.

"Tunamuomba waziri wetu Lukuvi awe na jicho la huruma aje atengue kifungo hichi tulichofungwa cha kuzuiliwa kujenga kwenye maeneo yetu ambayo hata hivyo tayari yameshapimwa,wengi wetu hapa tumna hati na vibali vya kujenga ili tuondokana na hizi nyumba ambazo ni duni kwa maisha ya Mtanzania," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa mtaa huo, Hemedi Selemani, aliwataka wakazi hao kutovunja sheria na agizo lililotolewa na Waziri la kutojenga kwenye maeneo yao wakati serikali ikilishughulikia kwa ajili ya kuwawezesha kujenga.

"Mimi kama kiongozi wenu wa mtaa huu nitahakikisha ninawasiliana na uongozi husika wa ofisi ya ardhi, ili kumuomba waziri muhusika atengue kifungo hiki tulichonacho na watu waendeleze kujenga makazi yaliyo bora ukizingatia kuwa wengi wenu hapa tayari mna hali na vibali vya kujenga," alisema.

Naye Ofisa Mtendaji wa mtaa huo, Shamimu Mohamed, aliwataka wakazi hao kuwa na uvumilivu wakati serikali ikilifanyia uamuzi ya kuwawezesha kujenga maeneo yao ambayo yameonekana kuwa na dosari katika upimaji wa kampuni ambayo haitambuliwi kisheria na serikali.



Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu, akizungumza na waandishi wa habari jana, wakati akipongeza uteuzi uliofanywa na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar Zuberi, wa Masheikh wa mikoa na makatibu wa mikoa wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania. PICHA: PETER MKWAVILA

# Mwamko wa wakulima mazao ya kimkakati kichocheo sekta kilimo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWAMKO mkubwa wa wakulima katika mazao ya kimkakati umetajwa kuwa kichocheo cha kunyanyua sekta ya kilimo hasa vijijini, kwa kuwa itaongeza uchumi wafamilia na Taifa kwa ujumla.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo na Mbegu (TARI), Hombolo mkoani Dodoma, Dk. Lameck Makoye, wakati wa mafunzo maalumu kuhusu mazao ya kimkakati ili kuongeza uelewa kwa wakulima namna ya kulima kilimo chenye tija.

Kutokana na kauli mbiu ya serikali ya awamu ya tano kuwa ya uchumi wa viwanda, kilimo cha mazao ya kimkakati ikiwamo uwele, mtama na ulezi vimekuwa vikitumika katika kuandaa baadhi ya vinywaji maeneo ya viwandani, hivyo kuinua maisha ya mkulima.

"Kwa sasa kuna matumaini kwa kundi la wakulima hasa wadogo baada ya kuendesha mafunzo ya mara kwa mara zikiwamo semina za wazi na vitendo... hii inamsaidia kuwa na ujuzi wa ziada kwa sababu lengo letu tunataka kilimo cha kisasa chenye faida tuondokane na kulima kwa mazoea," alisema Dk. Makoye.

Aliongeza kwamba wamelazimika kuendesha mafunzo kwa wakulima baada ya kubaini wakulima wengi hususani maeneo ya vijijini wanapenda mazao hayo hasa mtama ambao mbali na kutumika kama chakula vilevile wanauza.

"Mazao haya yanastahimili ukame na yanachukua muda mfupi ikilinganishwa na mazao mengine, hii inakuwa na manufaa kwa mkulima pamoja na kusaidia kuwa na akiba ya chakula kuepuka janga la njaa na mkulima kupata fedha baada ya kuuza," alisema.

Naye Diwani wa Chahwa, Sospeter Mazengo, alisema kuna umuhimu wa wakulima wote kushirikiana na TARI wasilime tu kama ilivyozoeleka bali walime kwa malengo na kutambua faida ya mazao wanayoyalima.

"Pamoja na yote, binafsi nimejifunza huu mtama, una manufaa mbalimbali ikiwamo la utengenezwaji wa bidhaa mbalimbali sasa kama zao la hivyo linatengeneza bidhaa inayotambulika dunia nzima, tunaweza kuwashawishi wakulima kutanua wigo ili kuwauzia wenye viwanda," alisema Diwani huyo.

Elisha Mwaluko, mkulima kutoka Kata ya Ipala, Wilaya ya Dodoma Mjini, alisema walikuwa wanalima kilimo cha kawaida na cha mazoea, kitendo ambacho misimu yote wamekuwa wakipata hasara na njaa.

Kuhusu mpangilio wa mazao shambani, Agnes Mlowesi, mkulima, alieleza wakulima wengi vijijini walikuwa hawana elimu ya kilimo cha kisasa kutokana na kutofikiwa kwa urahisi na wataalamu.

"Lakini ujio wa TARI, umekuwa mkombozi kwa kuwapa mafunzo ya aina ya mazao ya kupanda pamoja na mfumo, malengo na namna ya kuwekeza katika kilimo," alisema.





## Jiji laanza ujenzi wa shule ya Kiingereza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya inaendelea na ujenzi wa shule mpya ya msingi ya mchepuo wa Kiingereza itakayogharimu zaidi ya Sh. milioni 350, hivyo kuifanya kuwa na shule nne za aina hiyo.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa shule hiyo iliyopewa jina la Chifu Rocket Mwashinga wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa iliyotembelea shule hiyo, Mwalimu Amina Mwilemi alisema inatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Mwilemi alisema baadhi ya majengo yameshakamilika, hivyo tayari wameshaanza kutangaza nafasi ili wanafunzi waanze kupokelewa na kuifungua.

"Shule hii imepewa jina la Chifu Mwashinga kama sehemu ya kumuenzi chifu wetu. Tunaendelea na ujenzi wa maeneo mbalimbali muhimu ili wanafunzi watakapoanza kupokelewa wasome katika mazingira rahisi," alisema.

Diwani wa Nsalaga, Daud Ngogo, alisema ujenzi wa shule hiyo katika eneo hilo itakuwa chachu ya maendeleo ya shule zingine za msingi katika kata yake

Alisema majengo ya shule hiyo ni ya kisasa na yanavutia wanafunzi kusoma hivyo akawataka wananchi wa Kata hiyo kuitumia shule hiyo kama sehemu ya kujifunzia kwenye uboreshaji wa majengo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa shule hiyo huku akidai kuwa Serikali itaendelea kujenga shule za aina hiyo ili kuwasaidia wazazi ambao hawana uwezo wa kuwapeleka watoto wao kwenye shule za watu binafsi.

Alisema baada ya kumaliza ujenzi wa shule hiyo, Halmashauri hiyo itaanza ujenzi wa shule nyingine ya aina hiyo katika Kata ya Iwambi jijini humo na baadaye wataendelea na maeneo mengine.

Kutokana na ufinyu wa maeneo ya shule hizo, alisema wameanza kujenga madarasa kwa mfumo wa ghorofa ili kukabiliana na ufinyu wa maeneo hayo.

"Tumeanza kujenga maghorofa pale Shule ya Mkapa, kuna watu walisema hatuwezi lakini baada ya Mkurugenzi kwenda na wataalamu wake kwa ushauri wa Katibu Tawala iliwezekana na sasa ghorofa linaendelea kupanda," alisema Chalamila.

Baadhi ya madiwani wa Halmashauri ya Jiji, waliwashauri wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao katika shule hiyo ili wapate msingi mzuri wa elimu.

# Wavuvi hatarini kupata magonjwa mlipuko

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

WAVUVI na wafanyabiashara wa samaki kwenye mwalo wa Kafyofyo ulioko Ziwa Nyasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, wako hatarini kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na kutokuwa na vyoo.

Kutokana na hali hiyo, wananchi hao wanalazimika kujisaidia vichakani hali ambayo inasababisha vinyesi kusombwa na maji ya mvua na kuchanganyika kwenye mito na ziwa.

Hayo yalibainika juzi baada ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, timu ya wataalam wa afya na wakusanyaji wa mapato, kutembelea mwalo wa Kafyofyo kuangalia hali halisi ya eneo hilo.

Baada ya kujiridhisha kwamba hakuna vyoo na wakazi wa eneo hilo wakiwamo wavuvi na wafanyabiashara kujisaidia vichakani alitoa maelekezo kujenga vyoo vya muda wakati wakisubiri msimu wa mvua kumalizika na ushauri wa kitaalam kujenga vyoo bora vya kudumu.

Simon Josephat, mkazi wa Kijiji cha Kajunjumele, ambaye ni mchuuzi wa samaki na msanii wa kizazi kipya, alisema hali ya mwalo wa Kafyofyo si nzuri kutokana na kutokuwa na hakuna vyoo, hivyo kusababisha watu kujisaidia vichakani.

"Hali ya Kafyofyo si nzuri wananchi wanalazimika kujisaidia vichakani kwenye mito na ziwa kutokana na kukosekana na vyoo. Msimu huu wa mvua hata tukichimba vyoo vinabomoka kwa sababu ya mmomonyoko wa udongo," alisema Josephat.

Atupakisye Amon, mfanyabiashara eneo la Kafyofyo, alidai wameizoea hali hiyo ya kuendelea kujisaidia vichakani na kwamba baada ya mwenyekiti wa halmashauri na timu ya wataalam wa afya kuwatembelea kuwahamasisha kujenga angalau vyoo vya muda, wameanza utekelezaji.

Alisema mwalo wa Kafyofyo ni eneo ambalo linakusanya watu wa aina mbalimbali hivyo kukosekana kwa huduma ya vyoo kunahatarisha afya za wananchi.

Amon aliiomba serikali kuliangalia kwa jicho la pekee eneo hilo ambalo ni chanzo cha mapato kutokana na shughuli mbalimbali zinazofanyika ikiwamo uvuvi na biashara.

Pia alisema wananchi wahamasishwe kujenga vyoo bora vya kudumu na ikiwezekana serikali ijenge ili kukusanya fedha kwa watakaokuwa wanavitumia.

Aliongeza kuwa mwalo kwa Kafyofyo ni eneo ambalo wavuvi hawajajenga makazi ya kudumu kutokana na kazi yao kuwa ya kuhamahama.

Kingamkono alisema leo atapokea ripoti kutoka kwenye kamati ya fedha na mipango ili kubaini utekelezaji wa ujenzi wa vyoo vya muda kwenye mwalo wa Kafyofyo na namna ya kuondoa tatizo la ukosefu wa vyoo.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Saimon (kulia), akiwa amembeba mmoja wa watoto watatu mapacha wa Sara Shaban (wa pili kulia), waliozaliwa katika Hospitali ya Wilaya hiyo, mkoani Mbeya. Kushoto ni Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Michombelo Anaklet. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# DC aagiza uangalizi mama aliyejifungua watoto watatu

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, imemwagiza ofisa ustawi wa jamii wa wilaya hiyo kufuatilia kwa miezi sita malezi ya watoto watatu mapacha waliozaliwa wilayani humo ili kuhakikisha wanakuwa na afya njema.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Mayeka Simon, alitoa agizo hilo jana wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ilipofanya ziara ya kumtembelea mama wa watoto hao, Sara Shaban katika hospitali ya wilaya ambako amelazwa.

Simon alisema watoto hao watakabidhiwa rasmi kwa wazazi wao baada ya miezi sita na kwamba aliamua kutoa agizo hilo baada ya kubaini kuwa familia hiyo haina uwezo wa kiuchumi wa kuwatunza watoto hao. Aidha alimwagiza Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya, Omary Kapange, kuboresha mazingira ya nyumba ya familia hiyo iliyoko katika Kijiji cha Mbigwa kwa maelezo kuwa alibaini mazingira si mazuri kwa ustawi wa watoto hao.

Simon alisema alibaini kuwa nyumba ya familia hiyo inaingiza baridi, ina dirisha dogo linalosababisha hewa kuwa ndogo na hawana kitanda wala godoro hali ambayo haiwezi kuwa nzuri kwa ustawi wa watoto. "Hakikisheni mnaboresha mazingira ya nyumba ya familia hii. Huyu mama atabaki hapa hospitalini mpaka mazingira yaboreshwe na mtaendelea kufuatilia maendeleo mpaka baada ya miezi sita ndipo tutaiagiza rasmi familia hii," alisema Mayeka.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya, Dk. John Gungumka, alisema walimpokea mama huyo baada ya kupewa rufani kutoka katika zahanati ya Kijiji cha Mbigwa na walipompima walibaini kuwa alikuwa na watoto watatu.

Alisema mama huyo alijifungua watoto hao salama na kwamba yeye pamoja na watoto wake wanaendelea vizuri kiafya na wanaendelea kufuatilia afya zao kila siku.

"Alijifunga mtoto wa kwanza akiwa na kilogram 2.6 wa pili alizaliwa na kilogram 2.2 na wa tatu alikuwa na kilogram mbili. Awali tulikuwa hatujajua kama amebeba mapacha lakini tulibaini baada ya kumpima kwenye kipimo cha 'ultra sound'," alisema Dk. Gungumka.

Akizungumza mbele ya kamati ya ulinzi na usalama, mama wa watoto hao, alisema ana umri wa miaka 30 na uzao huo ni wa sita katika maisha yake na mpaka sasa ana watoto wanane.

Alisema awali alijifungua mapacha wawili ambao mmoja wao alifariki dunia na mmoja bado yupo na kwamba wengine walizaliwa mmoja mmoja kabla ya kujifungua watoto hao watatu.

Aliiomba serikali na wadau mbalimbali kumsaidia kwenye malezi ya watoto hao kwa madai kuwa hana maziwa ya kutosha kwa ajili ya kuwanyonyesha, hivyo akadai kuwa atalazimika kutumia maziwa mbadala.

Baadhi ya wadau wilayani hapa wameanza kujitokeza kumsaidia mwanamke huo kwa kumpatia fedha na vitu mbalimbali kwa ajili ya malezi.





## Wakulima kuhakikishiwa urahisi huduma pembejeo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WILAYA ya Kaskazini 'B' Unguja imejipanga kuhakikisha wakulima wanaondokana na changamoto ya huduma za kilimo ikiwamo pembejeo za kilimo na kurahisisha upatikanaji wake kwa wakati. Mkuu wa wilaya hiyo, Aboud Hassan Mwinyi, alisema hayo alipokuwa akizungumza na wananchi na wakulima wa Shehia za Donge Mtambile na Njia ya Mtoni katika ziara za kujitambulisha na kusikiliza kero za wananchi wa shehia hizo.

Alisema katika kipindi cha uongozi wake atahakikisha anasimamia suala la wakulima wa wilaya hiyo wanalimiwa kwa wakati na wanapatiwa pembejeo za kutosha ikiwamo mbolea kwa muda mwafaka.

Alisema endapo wakulima watalimiwa kwa wakati na kupata pembejeo nyingi kama inavyoshauriwa na wataalamu wa kilimo, hali hiyo itawasaidia wakulima kuvuna mazao mengi kutokana na kulima ndani ya msimu husika wa kilimo.

Akijibu malalamiko ya baadhi ya wakulima kuchukuliwa mashamba yao, Mkuu wa wilaya alisema wilaya hiyo imo katika utaratibu wa mipango miji ili kuhakikisha kila kitu kinawekwa sehemu yake na kufuata utaratibu uliowekwa na serikali hasa katika uendeshaji wa shughuli za kilimo.

Mkuu wa wilaya alisema mbali na matatizo yanayowakabili wakulima katika dhana za kilimo na pembejeo, lakini pia kuna tatizo la wakulima na wafugaji kufunga mifugo yao katika mashamba yenye vipando jambo ambalo huleta migogoro ya mara kwa mara na kuahidi kuishughulikia kero hiyo.

"Tatizo la migogoro ya wakulima na wafugaji linapaswa kushughulikiwa kwa haraka kabla halijaota mizizi na kuleta athari kwa pande zote mbili, lakini mbali na tatizo hilo pia tatizo la wizi wa mazoa nalo limekuwa sugu na watuhumiwa tunawaficha kwa kuwa ni jamaa zetu hivyo sitalifumbia macho," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi kilimo wa Baraza la Mji wilaya, Fatma Hamza Muhamed, alisema kuna usumbufu mkubwa katika upatikanaji wa pembejeo za kilimo pamoja na matrekta kwa sababu vinahitaji idhini ya moja kwa moja kutoka wizara ya kilimo.

# Makamu wa Pili wa Rais ahimiza nguvu ya pamoja miradi maendeleo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wananchi waendelee kushirikiana na serikali kwa kuongeza nguvu za pamoja zitakazowawezesha kukamilisha kwa wakati miradi ya maendelelo inayoanzishwa na serikali kwa faida yao.



Mkurugenzi Tiba wa Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Juma Salum Mbwana (kulia), akitoa maelezo kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman (kushoto), kuhusu kuanza kwa ujenzi wa mradi wa Hospitali ya Chake Chake, juzi. PICHA: OMPR-ZANZIBAR

Aliyasema hayo juzi wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya kilomita 9.3 iliyoanzia Kijiji cha Kipapo hadi Wambaa, akikamilisha ziara yake ya siku tano kukagua shughuli za maendeleo ndani ya wilaya nne za kisiwa cha Pemba, ameeleza kuridhika na mradi huo.

Hemed alisema dhima ya Serikali Kuu ni kuona matumaini ya wananchi katika kustawisha maisha yao yanafikiwa na kuimarika ili malengo waliyoyakusudia wakati wa kutoa ridhaa yao yafikiwe kwa nguvu kubwa.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo ikiwa ni ahadi za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi wakati wa kampeni zake za uchaguzi utaleta faraja kwa wananchi wa maeneo hayo hasa wakati wa msimu wa mvua ya masika wajawazito walipokuwa wakienda kujifungua.

Alizipongeza Taasisi na jumuiya za kiraia akitoa mfano wa Milele Foundation kwa moyo wao wa imani waliouonyesha wa kusaidia ufadhili wa ujenzi wa barabara ya Birikau yenye urefu wa kilomita 4.3.Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kamwe haiwezi kudharau jitihada zinazofanywa na taasisi na jumuiya za kiraia na kuwaahidi wawakilishi wa taasisi hizo kuwa serikali iko tayari kushirikiana nazo wakati wote ili yale malengo ya misaada wanayotoa kwa ajili ya jamii yafanikiwe.

Aliwataka vijana wanaobahatika kupata fursa za ajira kwenye miradi ya maendeleo wenye tabia ya wizi kuacha udokozi wa vifaa vya miradi ya serikali na badala yake wajenge utamaduni wa kutoa taarifa unapotokea wizi au ubadhirifu na serikali itakuwa tayari kutoa zawadi kwa vijana watakaojitokeza.

Ofisa Mdhamini Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Pemba, Ibrahim Saleh Juma, alimweleza Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwamba barabara ya kilomita 9.3 ya Kipapo hadi Wambaa imeshakamilika kwa awamu mbili za kifusi kilichofikia urefu wa kilomita sita hadi sasa.

Ibrahimu Saleh, alisema madaraja manne yatahusisha ujenzi huo unaotarajiwa kukamilika kwa kiwango cha lami ikisubiriwa kupisha kwa msimu wa mvua kuanzia masika.

Akikagua mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Chake Chake, Makamu wa Pili wa Rais, aliwaagiza wahandisi wa ujenzi wa mradi huo Kampuni ya Runs kuendeleza tena ujenzi huo ndani ya saa 24 baada ya kusita kwa takriban miezi mitatu.Alisema kazi lazima iendelee kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa kwa vile malipo ya ujenzi huo yameshafikia asilimia 30 wakati kazi inayoendelea kwa sasa ina asilimia 25.

Wakati huo huo, Hemed Suleiman, alitembelea mradi wa vijana wa kilimo cha Kisasa (Green House) uliopo katika Kijiji cha Mjini Ole, ambao umeanza mwaka 2018.

Alisema wananchi wana wajibu wa kutunza fedha na mali za serikali zinazotolewa kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo na aliwaahidi vijana hao kwamba viongozi wa kitaifa kwa kushirikiana na wa jimbo watalipatia ufumbuzi tatizo la sehemu ya ufugaji kuku.

# Wananchi wataka adhabu iongezwe makosa udhalilishaji

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKAZI wa Shehia ya Mtambwe Kaskazini, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, wamesema vyombo vya sheria kuendelea kutoa adhabu ndogo kwa watuhumiwa wa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ndicho chanzo cha matendo hayo kuendelea kuongezeka na kusababisha athari zaidi katika jamii.

Walisema hayo jana wakati wa mkutano wa kamati za kupinga udhalilishaji Wilaya ya Wete, wenye lengo la kuhamasisha jamii kuhusu masuala ya kupinga udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo elimu ya namna ya kuibua na kufuatilia kesi hizo katika vyombo vya sheria.

Othman Haji Kibano, akizungumza katika mkutano huo ulioratibiwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, Zanzibar (TAMWA -ZNZ), alisema licha ya juhudi zinazochukuliwa na wanajamii kuripoti taarifa za matukio hayo yanapojitokeza, mwenendo wa hukumu na adhabu ndogo kwa watuhumiwa zinawakatisha tamaa na kusababisha wadhalilishaji kuendelea na vitendo hivyo bila hofu.

"Wanajamii tunajitahidi sana kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za vitendo hivi, lakini tukimpeleka mtuhumiwa leo polisi cha kushangaza baada ya siku tatu tunamuona amerudishwa mtaani, hii inatuvunja sana moyo kwani sisi ndio tunaoumia huku mtaani," alisema.

Naye Hamad Idd Hamad alisema; "Kama kweli serikali inataka vitendo hivi vimalizike katika jamii basi wasiwaachilie huru watuhumiwa hawa kwa adhabu ndogo kwani kunawafanya hawajutii na matokeo yake wanarudia na kuendelea kuharibu watoto wetu."

Alisema kutokana na mwenendo wa watuhumiwa kuachiwa huru husababisha baadhi yao kukata tamaa ya kuripoti kesi hizo jambo ambalo linahatarisha zaidi usalama wa watoto.

Mapema Ofisa ustawi wa jamii Wilaya ya Wete, Haroub Suleiman Hemed, alisema jamii haipaswi kukata tamaa utoaji taarifa za matendo hayo kwa kuwa kufanya hivyo kutazidi kuwapa nguvu wadhalilishaji kuendelea kuharibu watoto bila hofu.

"Watu wengi wanadhani kwamba njia sahihi baada ya kutokea tukio la udhalilishaji ni kukaa na kumaliza nyumbani, hawaangalii madhara yanayompata mwathirika, nikuombeni tuache tabia hizi kwa kuwa kufanya hivyo tunawaweka watoto wetu katika hatari zaidi ya kufanyiwa udhalilishaji," alisema.

Mkuu wa Upelelezi na Mratibu wa Dawati la Kijinsia kutoka Jeshi la Polisi Wete, Fakih Yusuf Moh'd, aliwataka wanajamii kutoa ushirikiano wa taarifa linapotokea tukio ili uchunguzi uweze kufanyika kwa wakati na mtuhumiwa achukuliwe hatua kisheria.

"Tunafahamu kuna baadhi ya askari si waadirifu sana, lakini nakuombeni, ukimwona askari polisi anakushawishi upatane na mdhalilishaji ili kuimaliza kesi kataa, sisi jeshi la polisi tunahitaji taarifa kutoka kwenu ili tufanye kazi yetu, hii kazi haihitaji muhali kufanikiwa kwake," alisema.

Juma Musa Omar, kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Wete, alisema serikali kupitia ofisi hiyo imeweka mkakati maalum wa kuzisimamia kesi za udhalilishaji ili kuhakikisha zinapata hukumu na watuhumiwa watumikia adhabu kwa mujibu wa sheria.

"Sisi DPP tuna mkakati maalumu tunaokwenda nao, sasa hatufuti kesi hata moja ya udhalilishaji kwa mtu anayekuja kutaka tuifute kesi hiyo, au anayegoma kuja mahakamani kutoa ushahidi, kwani tumegundua wengi wanatumia mwanya huo wa kutokwenda kutoa ushahidi ili muda ukifika kesi yao ifutwe," alieleza.

Mratibu wa TAMWA Zanzibar ofisi ya Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema mkutano huo ni mwendelezo wa juhudi za TAMWA ZNZ kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupambana na vitendo vya udhalilishaji katika jamii kwa kuwawezesha elimu ya ufuatiliaji na utoaji wa ushahidi mahakamani ili kujenga jamii yenye kuzingatia usawa na usalama wa kila mmoja.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

Nafasi za Kazi ualimu diploma science/math/IT 0715382833

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA INA VYUMBA VIWILI IPO KIJITONYAMA PLOT NAMBA 712/1 BLOCK 46 DAR ES SALAAM BEI 300M,MAZUNGUMZO YAPO.

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**KATIKA MAHAKAMA KUU TANZANIA**
**ARUSHA**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 6 LA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**RICHARD NKINGWA**
**KWITERA...............MAREHEMU**
**NA**
**JANETH GEORGE MUKARA**
**........................MSIMAMIZI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75).**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia maombi haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mpingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 3 Mwezi wa Tano mwaka 2021.

Imewasilishwa Arusha leo tarehe 1 Mwezi wa Nne mwaka 2021

**R.B. Massam**
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU**
**ARUSHA.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**RACHEL ZAKAYO SWALLO** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo, cheti cha kidato cha nne chenye index namba P1157-0030 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **IWAWA mwaka 2007** na cheti cha chuo cha **UALIMU(MBEYA LUTHERAN TEACHER'S COLLEGE)** chenye namba **E0548-0096** kilichotolewa mwaka **2010**,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **MKB/RB/2670/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GEOFREY E. NTIGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3349/0036** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **KOLANDOTO SEKONDARI** mwaka **2017**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **SHY/RB/627643/2020.**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT DODOMA**
**MISCELLAOUS LAND REVISION NO 8 OF 2020**
**AMINA RAMADHANI APPLICANT**
**VERSUS**
**ATHUMAN HINGA &ANOTHER RESPONDENT**
**TO. YAHAYA M. SINGU**

**NOTICE OF DATE OF HEAR/MENTION.**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for/hearing/mention on **16 days of 4 2021** at 9:00am.

Before **Hon. L. MANSOOR JUDGE**

**YOUR ARE** required to appear in his Court on the fixed date without fail. And you may bring with you all required document in support of your case.

Given under my hand and the seal of the Court this 29 days of 3 2021.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.91/2021**

Ombi la Mwantumu Hassan Chando Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu Rajabu Said Samatha

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 18/05/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 08/04/2021

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY**
**AT DAR ES SALAAM**
**MATR/MISC,CIVIL/PROB**
**&ADMIN/CIVIL/APPL/APPEAL/CAUSE/REV/REVIEW/CAUSE**
**5 OF 2020**
**ALI SAMIR**
**YOUSSEF............PLANTIFF/APPEALANT**
**VERSUS**
**EUNICE SHAUNDRE**
**CLEOTE...............DEFENDANT/RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE OF MENTION**

TAKE NOTICE that the above mentioned case has been fixes for mention/hearing/first PTC/final PTC on 27th day of APRIL year 2021 at 11:00 AM before Hon LM.MLACHA judge

YOU ARE required to appear in this court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

GIVEN under my HAND and the SEAL of the COURT this 17th day of MARCH year 2021

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wiliaya ya**
**MOROGORO kituo KINGOLWIRA**
**Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi No 6/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**GILBERT EMMANUEL MSHANA WA MISUFINI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA**
**MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA**
**DANIEL GILBERT MSHANA**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote / maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa

Hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri Hili Endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo

Tarehe 6 mwezi 5 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuleta Mahakamani kukaguliwa.

*Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa.

*Marehemu hakuacha wosia

*Futa isiyohusika

Imetolewa leo Tarehe 6 mwezi 4 Mwaka 2021

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**HUSSEIN IDD RAJAB.** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye jina la **CITY BOYS ELECTRONICS CO LTD.** yenye namba za usajili **MC 671 BDT.**Chassis **No.MD6M14PK5F4L21667,** Engine **No. OK4LF4294052** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/RB/5372/2021.**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mfumuko wa bei wapungua

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFUMUKO wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Machi 2021, umepungua kutoka asilimia 3.3 kwa mwaka mwezi February 2021, hadi asilimia 3.2 kwa mwaka, Machi 2021.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dodoma na Mkurugenzi wa sensa ya watu na takwimu za jamii, Ruth Minja, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

"Hii inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Machi 2021, imepungua ikilinganishwa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia mwezi Februari, mwaka huu," alisema.

Alisema kupungua kwa mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Machi, mwaka huu kumechangiwa na kupungua kwa bei za bidhaa zisizo za vyakula kwa kipindi kilichoishia mwezi Machi mwaka huu, zikilinganishwa na bei za Machi, mwaka jana.

"Baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilipungua bei kwa mwezi Machi mwaka huu zikilinganishwa na bei za mwezi Machi mwaka Jana ni pamoja na dizeli kwa asilimia 17.7, mafuta ya taa kwa asilimia 13.5, petroli kwa asilimia 8.0 na gesi ya kupikia kwa asilimia 4.1," alisema Minja.

Alisema kwa upande mwingine mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwezi Machi mwaka huu umeongezeka kutoka asilimia 3.6 mwezi februari mwaka huu hadi asilimia 4.3.

"Mfumuko wa bei ambao haujumuishi vyakula visivyochakatwa, nishati na bili za maji (Core inflation) kwa mwezi Machi, mwaka huu, umebaki kuwa asilimia 3.6 kama ilivyokuwa mwezi Februari, mwaka huu,"alisema.

**MFUMUKO WA BEI AFRIKA MASHARIKI**

Alisema kuwa nchini Kenya mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Machi, mwaka huu umeongezeka kutoka asilimia 5.78 kwa mwaka ulioishia mwezi Februari mwaka huu hadi asilimia 5.90 kwa mwaka ulioishia mwezi Machi, mwaka huu.

Kwa upande wa Uganda mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Machi, mwaka huu umeongezeka kutoka asilimia 3.8 kwa mwaka ulioishia mwezi Februari hadi asilimia 4.1.

# Ummy aja na mwarobaini wa wanafunzi kukaa chini ya miti

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ameagiza kuwekwa mikakati ya kumaliza tatizo la watoto kukaa chini ya mti.

Akizungumza na menejimenti ya ofisi yake jana, wakati wa kuwapokea Katibu Mkuu Prof. Riziki Shemdoe na Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Afya, Dk. Grace Magembe, Waziri Ummy alisema ni marufuku watoto wa Kitanzania kusomea chini ya miti.



"Rais Samia Suluhu Hassan ametoa maelekezo kuwa hataki kuona mtoto wa Kitanzania akisoma chini ya mti, hivyo TAMISEMI ina wajibu wa kutekeleza maagizo hayo kwa kuweka mikakati thabiti ya kutatua kero hiyo," alisema.

Aliwataka atendaji wakuu wa wizara kuanza utekelezaji wa maagizo hayo ili kuondoa tatizo hilo sambamba na kumaliza mlundikano wa wanafunzi darasani lengo likiwa kuboresha mazingira mazuri ya kujifunzia.

Kuhusu mlundikano wa wanafunzi darasani, Ummy alisema inasikitisha kuona baadhi ya shule nchini zina mlundikano mkubwa wa wanafunzi, hali hiyo ni hatarishi kwa wanafunzi na inapunguza uelewa katika masomo.

"Napata taabu sana kuona watoto wanakaa 200 katika darasa moja na baadhi ya shule watoto wanabadilishana wengine wanakuja asubuhi na wengine mchana kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Siamini katika hilo kwa kuwa watoto wanaoingia mchana haweze kuwa makini katika kusoma lazima tubadilishe kwa kujenga vyumba vya madarasa vya kutosha.

"Ni wakati sasa wa kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kutatua changamoto hizo kwa kusimamia ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri ili kufanikisha kazi hizi muhimu katika kukuza sekta ya elimu nchini," alisema.



Wananchi wakijiandaa kusaidia kulinasua lori lililokuwa limekwama katika barabara mbovu ya Matosa, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ripoti: Mabilionea Afrika wapungua

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

IDADI ya Waafrika imepungua kwenye orodha ya mabilionea wa dunia, huku mfanyabiashara Mohamed Dewji, maarufu Mo, akiwa bilionea pekee kutoka Afrika Mashariki aliyepenya kwenye orodha hiyo.

Kwa mujibu wa ripoti ya jarida la mambo ya kibiashara la Forbes iliyotolewa juzi, Afrika inajivunia mabilionea 18 waliochomoza safari hii kwenye mabilionea dunia, utajiri wao wote kwa ujumla ukiwa Dola za Marekani bilioni 74.

Kwa mujibu wa orodha hiyo , Aliko Dangote wa Nigeria (pichani) anaendelea kuongoza kwa utajiri kwa mwaka wa 10 mfululizo akiwa na ukwasi wa dola bilioni 11.6. Hata hivyo, Dangote ni wa 190 katika orodha ya matajiri wa dunia nzima.

Barani Afrika, Dangote alifuatwa na Nassef Sawiris wa Misri mwenye utajiri wa Dola bilioni 8.5, Nicky Oppenheimer wa Afrika Kusini akiwa na utajiri wa Dola bilioni 8.0, Johann Rupert wa Afrika Kusini Dola bilioni 7.2 na Mike Adenuga wa Nigeria mwenye utajiri wa Dola bilioni 6.3.



Kwa Afrika Mashariki, Mtanzania Mo Dewji pekee ndiye aliyeingia katika orodha hiyo.

Ingawa idadi ya matajiri hao katika Jarida la Forbes iliongezeka kote duniani, ikiweka rekodi kwa kuongeza watu wapya 493, idadi ya mabilionea wa Afrika ilipungua ikilinganishwa na mwaka 2020 ilipokuwa 20.

Mabilionea 18 wa Afrika wanatoka mataifa mbalimbali kama vile Afrika Kusini na Misri zikiwa na matajiri watano kila moja, Nigeria watatu, Morocco wawili, Zimbambwe, Tanzania na Algeria zina tajiri mmoja.

# TUCHEL AFUNGUKA KUWATOA HAVERTZ, WERNER




**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amebainisha, Kai Havertz na Timo Werner walitolewa nje kwa sababu hawakuwa kwenye viwango bora, katika mchezo wa ushindi wa robo fainali wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Porto, Jumatano.

Mason Mount na Ben Chilwell kila mmoja alifunga bao moja kwenye ushindi wa mabao 2-0 wakati Chelsea wakiondoka na pointi zote tatu kwenye mchezo huo wa kwanza mjini Seville.

Ilikuwa siku nzuri kwa Tuchel, ambaye kikosi chake cha watu 10 kilikumbana na kipigo kikali cha mabao 5-2 kutoka kwa West Brom kwenye Ligi Kuu England mwishoni mwa wiki.

Havertz na Werner hawakuwa kwenye kiwango bora na raia hao wa Ujerumani walitolewa nje na nafasi zao kuchukuliwa na Olivier Giroud na Christian Pulisic huku zikiwa zimesalia dakika 25 mchezo kumalizika na Tuchel ameelezea mabadiliko hayo.

Katika mechi 29 za mwisho kwenye mashindano yote, Werner amekosa nafasi kubwa 20.



# Neymar afungiwa mechi mbili

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR amefungiwa kuichezea Paris Saint-Germain mechi mbili zijazo za Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Shirikisho la Soka la Ufaransa (LFP), limetangaza.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil alitolewa nje baada ya kuzozana na mlinzi wa Lille, Tiago Djalo, ambaye pia alilimwa kadi nyekundu.

Neymar na Djalo awali walikuwa wafungiwa mechi tatu, lakini wakapunguziwa moja kila mmoja.

Kichapo cha Jumamosi cha bao 1-0, kimeiacha PSG ikipitwa pointi tatu na Lille walioko kileleni mwa msimamo wa Ligue 1 na wakiwa pointi moja juu dhidi ya Monaco iliyopo nafasi ya tatu.

Kikosi hicho cha kocha, Mauricio Pochettino, kitakuwa bila Neymar kwa mechi za wikendi dhidi ya Strasbourg ugenini na nyumbani dhidi ya Saint-Etienne, Aprili 18, mwaka huu baada ya mchezo wa pili wa robo fainali wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich.

Viungo wa PSG, Leandro Paredes na Idrissa Gueye pia hawatakuwapo kwenye mchezo dhidi ya Strasbourg kutokana na kuwa na kadi nyingi za njano.

# Boateng sasa rasmi kuondoka Bayern

**MUNICH,** Ujerumani

JEROME Boateng hatapewa mkataba mpya wa kuendelea kucheza Bayern Munich mwishoni mwa msimu huu, Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Hasan Salihamidzic ametangaza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 ametumia misimu 10 akicheza hapo kwenye dimba la Allianz Arena, akicheza mechi zaidi ya 350 kwa kipindi alichokaa hapo na kushinda mataji 21.

Alikuwa chaguo la kwanza kwa Bayern msimu uliopita wakati wakishinda mataji matatu na alianza katika mechi 29 kwenye mashindano yote.

Hata hivyo, wakati Dayot Upamecano, akiwa anajiandaa kutua hapo akitokea RB Leipzig msimu ujao, nyota huyo wa zamani wa Hamburg na Manchester City atafuata nyao za mlinzi mwenzake, David Alaba, kuondoka hapo mara mkataba wake utakapofikia mwisho.

"Mkataba wa Jerome unamalizika kipindi cha majira ya joto kijacho na hatutamwongezea," alisema Salihamidzic akiiambia Sky Sport Germany kabla ya mchezo wa Jumatano wa Ligi ya mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain ambao walichezea kichapo cha mabao 3-2.

"Anaondoka kwenye mlango mkubwa, kwa matumaini akiwa na mataji mengi zaidi."

Majaliwa ya Boateng yalianza kuzua uvumi ndani ya klabu hiyo, baada ya kuripotiwa kwamba, hana uhusiano mzuri na Salihamidzic pamoja na kocha mkuu Hansi Flick.

Mlinzi huyo wa kati pia ameichezea Ujerumani mechi 76, lakini pia hajaitwa kwenye kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Joachim Low tangu Oktoba, mwaka 2018.

Alaba alitangaza Februari, mwaka huu kuwa ataondoka Bayern wakati mkataba wake utakapofikia mwisho ifikapo Juni.



HABARI MICHEZO

# De Bryune kuikamua Man City mshahara

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester City, Kevin de Bruyne, amesaini mkataba mpya utakaomweka klabuni hapo hadi mwaka 2025.

De Bruyne mwenye umri wa miaka 29, ni mchezaji mwenye ushawishi mkubwa klabuni hapo na mkataba wake wa sasa ulikuwa unamalizika mwaka 2023.

Hivyo mabosi wa Manchester City wameamua kumwongezea miaka miwili zaidi kwenye mkataba wake wa sasa ili aendelea kubakia hapo kwenye dimba la Etihad.

Baada ya kusaini mkataba huo nyota huyo amemaliza uvumi wa kuwa anaweza kuondoka klabuni hapo, kutokana na mazungumzo yaliyofanyika siku za nyuma kushindwa kufikia mwafaka hasa kwenye suala la mshahara.

Tangu atue City akitokea Wolfsburg mwaka 2015, De Bruyne amecheza michezo 254 na mkataba wake huo mpya utamfanya kuvuta mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki.





# KONATE: WERNER NI HATARI KULIKO HAALAND

**DOTMUDN,** Ujerumani

MLINZI wa RB Leipzig, Ibrahima Konate, amemtaja mshambuliaji wa Chelsea, Timo Werner, kama mchezaji hatari zaidi kukutana naye ukilinganisha na Erling Haaland.

Konate anacheza katika Ligi Kuu Ujerumani pamoja na Halaanad ambaye yupo pale Borussia Dortmund, huku Warner pia alicheza huko kabla ya kutimkia Ligi Kuu England.

Konate aliulizwa na Bild kuhusu mshambuliaji gani hatari zaidi kukutana naye kati ya Robert Lewandoski, Werner na Haaland.

Na Konate akaweka wazi kwamba, Werner ni hatari zaidi linapokuja suala la kukabiliana ana kwa ana.

""Werner kwangu mimi ni mshambuliaji hatari zaidi kuliko Halaand, maana ni ngumu sana kumkabili."

Werner ameifungia Chelsea na Ujerumani mabao mawili katika michezo 31 ambayo ameichezea mpaka sasa, wakati Haaland amefunga mabao 33 katika michezo 33 akiwa na Dortmund pekee.

Konate alikuwa Werner katika kila wiki za mazoezi walipokuwa pamoja katika klabu ya Rb Leipzig, wakiwa wamecheza mechi 57 pamoja katika misimu mitatu waliocheza pamoja.

# *Everton yamweka sokoni Mina*

**LIVERPOOL,** England

EVERTON wameweka wazi wapo tayari kumuuza mchezaji wao, Yerry Mina katika dirisha la uhamisho lijalo ikiwa ofa itakayowasilishwa itaendana na dau wanalolitaka wao la kuanzia la pauni milioni 21.

Kwa mujibu wa Tuttomercatoweb, Everton hawajizuii kumuuza Mina ili waweze kupata nafasi na fungu la kuongeza nguvu katika usajili wa wachezaji bora zaidi, wenye uwezo na uzoefu mkubwa.

Taarifa zinasema Kalidou Koulibaly, ambaye alishawahi kufanya kazi na kocha Carlo Ancelotti pale dimbani Diego Armando Maradona katika timu ya Napoli, ni miongoni mwa wachezaji wanaotupiwa jicho.

Koulibaly anaweza kuwagharimu Everton kiasi cha pauni milioni 43, hivyo klabu inahitaji kutengeneza vyanzo zaidi kwa ajili ya kupata fedha hiyo na hiyo inawezekana kupitia kuwauza wachezaji kadhaa.

Hata hivyo, katika kuinasa saini ya mchezaji huyo, klabu itakayomtaka itakumbana na ushindani kutoka kwa Real Madrid, Liverpool na Manchester United.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# DEMBELE ACHOMOA KUSAJILIWA UNITED

## Ni baada ya winga huyo kusema bado anahitaji kuendelea kuitumikia klabu hiyo

**BARCELONA,** Hispania

WINGA Ousmane Dembele ameripotiwa kuwa hataki tena kuondoka Barcelona katika dirisha lijalo la uhamisho la majira ya joto, na kwamba hana mpango wa kujiunga na Manchester United.

**Nyota huyu amekuwa sehemu muhimu sana ya kikosi cha Barca kwa msimu huu 2020-21, akiwa amecheza jumla ya mechi 36 na kufunga mabao 10 na kutoa pasi za mwisho nne.**

Mkataba wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 upo mbioni kuisha ifikapo Juni, mwaka huu na United wamekuwa wakihusishwa zaidi kutaka kumsajili.

Walijaribu hivyo kipindi cha dirisha dogo la usajili la Januari, lakini waligonga mwamba, na wameripotiwa sasa wanaisaka tena.

United ilitaka kwanza imsajili kwa mkopo kipindi cha dirisha la uhamisho la majira ya joto lililopita, lakini Barcelona wakakataa dakika za mwisho.

Dembele anatambua kuwa United wamemweka kwenye rada zao, na wanafanya mipango ya kupata huduma yake, lakini gazeti la Mundo Deportivo limemnukuu akisema yeye bado hajataka kuachana na kikosi hicho cha Ronald Koeman.

Mashetani wekundu hao wanahitaji kupata mbadala wa huduma yake sokoni, hasa kwa kuzingatia Barcelona wanataka kulishikilia suala la mkataba mpya wa Dembele kama kipaumbele kwa sasa.

Taarifa zaidi zinasema Barcelona wametoa ofa ya mkataba mpya wa miaka mitatu kwa nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Dembele ambaye amecheza jumla ya mechi 110 na Barcelona na kufunga jumla ya magoli 29 na kutoa asisti 20 kwenye mechi 110, pia alizivutia baadhi ya klabu kutoka Serie A wakiwamo Juventus.

## ZISIKUPITE

### LINGARD ANG'ANG'ANIWA

WEST Ham itafanya vyovyote vile ili kumsajili kwa mkataba wa kudumu kiungo wa kati, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28 kutoka Manchester United. Kwa mujibu wa United, nyota huyo thamani yake ni pauni milioni 30. ***(Sky Sports)***

### ARSENAL YAMFUATA ZAHA

ARSENAL imerejesha nia yao tena ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Crystal Palace, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 28. ***(90min)***

### STERLING, FODEN KUMEKUCHA

MANCHESTER City wanalenga kukubaliana kuingia katika mkataba mpya na washambuliaji wa England, Phil Foden (20), na Raheem Sterling (26), kabla ya mwishoni mwa msimu. Hii ni baada ya kiungo wa kati wa Ubelgiji Kevin de Bruyne mwenye miaka 29, kuongeza mkataba wake hadi mwaka 2025. ***(Eurosport)***

### CITY YAMTOSA MESSI

MANCHESTER City haitamfuatilia mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi hadi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, atakapoweka wazi kuwa anataka kuondoka Barcelona. ***(Marca-in Spanish)***

### VESTERGAARD AWINDWA

KLABU ya Tottenham Hotspur itajaribu kumsajili mlinzi wa kati wa Southampton, Jannik Vestergaard mwenye umri wa miaka 28, ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 18. ***(Express)***

### KONATE MAMBO BADO

LIVERPOOL wameiambia RB Leipzig kuwa hawatamsajili mlinzi wa kati wa Mfaransa, Ibrahima Konate, mwenye umri wa miaka 21. ***(Bild, via Express)***

### LIVERPOOL, CHELSEA VITANI

LIVERPOOL watakabiliana na ushindani na Chelsea kwenye mbio za kuwania saini ya kiungo wa kati wa Ajax, Ryan Gravenberch mwenye umri wa miaka 18, ambaye anatazamwa kuwa mbadala wa Georginio Wijnaldum (30). ***(Gazzetta dello Sport,via Express)***

### KING AKARIBIA CELTIC

KOCHA wa zamani wa Bournemouth, anataka kumsajili mshambuliaji wa Everton, Josh King, mwenye umri wa miaka 29, kuwa mchezaji wa kwanza kumsajili akiwa kocha mpya wa Celtic. ***(Sun)***

### GRACIA AIGUSA BARCA

KLABU ya Barcelona inaendelea kumfuatilia mlinzi wa Manchester City, Eric Garcia, lakini wametoa ofa pungufu ikilinganishwa na iliyowekwa mezani dirisha la usajili la msimu uliopita. ***(Marca)***

### HERRERA KITAELEWEKA

KLABU za Southampton na West Ham ni miongoni mwa timu zinazovutiwa na kiungo wa kati wa Manchester City, Yangel Herrera, 23, ambaye anacheza kwa mkopo katika klabu ya Granada. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

# AZAM, MTIBWA SUGAR TAMBO ZATAWALA BARA

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Azam FC kinatarajia kuwakaribisha Mtibwa Sugar kutoka Manungu, Morogoro katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuwa na ushindani itakayochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

**Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, aliliambia gazeti hili kikosi chake kipo fiti kwa ajili ya kupambana kupata pointi tatu muhimu katika mchezo huo ambao wanafahamu hautakuwa mwepesi.**

Vivier alisema wamefanya maandalizi mazuri na katika kuwaweka tayari wachezaji wao, walicheza mechi mbili za kirafiki ambazo zimewapa matumaini ya kufanya vizuri katika mchezo huo.

Kocha huyo alisema pia mechi hizo za kirafiki zimewapa mwanga na kubaini upungufu yao ambayo tayari wameyarekebisha ikiwamo katika safu ya ushambuliaji na ulinzi.

"Ushambuliaji na ulinzi haukuwa vizuri huko nyumba, lakini kwa sasa hali sio mbaya katika nafasi hizo, ukiangalia kwenye mechi mbili za kirafiki tulizocheza zimetusaidia, tumefanikiwa kufunga mabao sita, mechi ilimalizika kwa 6-1, hivyo sio mbaya sana kwetu," alisema Vivier.

Hata hivyo aliweka wazi jana asubuhi kikosi chao kilishindwa kuendelea na mazoezi ya mwisho kwa ajili ya mvua kubwa iliyonyesha lakini jioni walitarajia kukamilisha programu za kuelekea mechi hiyo.

"Nina imani upungufu wetu wa ulinzi tumeufanyia kazi, hasa kujisahau tunapokuwa tunaongoza na kuwapa wapinzani nafasi ya kusawazisha, lakini pia safu ya ushambuliaji kuwa makini katika kumalizia nafasi zote tunazotengeneza," alisema kocha huyo.

Mtibwa Sugar wataendelea kumkosa kocha wao Mkuu, Thierry Hitimana kwa sababu ya kurejea kwao baada ya kutofautiana na msaidizi wake, Vincent Barnabas.

"Mkataba si tatizo sana, lakini kubwa lilikuwa ni kuingiliwa majukumu yangu na kutokuwa na ushirikiano na baadhi wa wenzangu kwenye benchi la ufundi, hivyo kama Mtibwa Sugar wananihitaji niendelee ni lazima waliondoe hili tatizo ili mimi nifanye kazi kwa uhuru, vinginevyo itakuwa ngumu kwa mimi kurejea," alisema Hitimana.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara Mtibwa Sugar iko katika nafasi ya 14 ikiwa na pointi 24 baada ya kucheza mechi 22 wakati Azam iko nafasi ya tatu baada ya kufikisha pointi 44 na ikishuka dimbani mara 24.



Wachezaji wa Yanga, Deus Kaseke (kulia) na Feisal Salum (katikati), wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# KMKM yajipanga kuitesa Mlandege

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kumalizika kwa maombolezo ya msiba wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli, 'Maafande' wa KMKM wanatarajia kuwakaribisha Mlandege katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa kwenye Uwanja wa Mau A, visiwani hapa.

KMKM ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 32 wakati wapinzani wao Mlandege wako katika mstari wa hatari wa kushuka daraja baada ya kuwa katika nafasi ya pili kutoka mkiani wakiwa na pointi 17 mkononi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu alisema wamejipanga kuendeleza kasi ya ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kunyakuwa ubingwa wa ligi hiyo katika msimu huu wa mwaka 2020/21.

Msimu alisema mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu kutokana na timu zote zimetoka katika mapumziko ya muda mrefu ambayo yamewasaidia kujiimarisha na hatimaye kutimiza lengo lake.

Alisema lengo la KMKM ni kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo lakini wanafahamu wapinzani wao wanahitaji kujinasua na janga la kushuka daraja.

"Tumejiandaa kupata alama tatu ili kujiweka katika sehemu nzuri ya kuendelea kubakia kileleni na kutimiza lengo la kunyakuwa ubingwa, hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu wapinzani wetu na wao wanahitaji kushinda, utulivu wa wachezaji na kufuata maelekezo ya walimu ndicho kitakachosaidia kutoka na ushindi," alisema Msimu.

Aliongeza lengo la KMKM ni kutaka kushiriki mashindano ya kimataifa na wanaamini wakipata nafasi hiyo wataiwakilisha vyema Zanzibar kwenye michuano hiyo.



# King Giovanni afariki, kuzikwa Sinza

**Na Sabato Kasika**

MAZISHI ya mpiga solo wa siku nyingi, King Giovanni, yanatarajiwa kufanyika kesho kwenye makaburi ya Sinza jijini Dar es Salaam baada ya mipango ya kusafirisha mwili kwenda kwao Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kukwama.

King Giovanni alifariki dunia mapema wiki hii, ikiwa ni siku chache baada kushiriki katika wimbo wa maombolezo wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa wanamuziki wa DRC wanaoishi hapa nchini, King Dodoo alisema mwili wa marehemu King Giovanni umehifadhiwa katika hospitali ya Mwananyamala na taratibu za kufanikisha mazishi hapa nchini zinaendelea vizuri.

"Mwanzoni tulipanga kusafirisha maiti hadi nyumbani kwao marehemu kule Lubumbashi, lakini kutokana na mambo ambayo yako juu ya uwezo wetu, tumeona tumzike tu hapa jijini Dar es Salaam," alisema King Dodoo.

Kiongozi huyo aliongeza kinachoendelea sasa ni kuandaa ratiba ya kutoa heshima za mwisho na mahali ambapo shughuli hiyo itafanyika ili kuhakikisha tunakamilisha mchakato huo siku ya Jumamosi.

"Ninaomba mashabiki wa muziki tuungane katika msiba huu ambao umeikumbuka tasnia yetu ili tuweze kumhifadhi mwenzetu katika nyumba yake ya milele pale Sinza," King Dodoo alisema .

Marehemu King Giovanni aliwahi kuwa kiongozi wa bendi ya Chu-chu Sound .

Michezo

Ijumaa Aprili 9, 2021

Nipashe



Dembele achomoa kusajiliwa United UKURASA 22



Kiungo wa Simba, Rally Bwalya (kulia), akijipanga kumtoka nyota mwenzake wa timu hiyo, Jonas Mkude, katika mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji Al Ahly, itakayochezwa leo kuanzia saa 4:00 usiku jijini Cairo, Misri. **PICHA: SSC**

## Yanga, KMC muda utaamua

**Na Saada Akida**

TAMBO na majigambo zinaendelea kutawala kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Yanga dhidi ya KMC FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh, aliliambia gazeti hili wachezaji wote wanaendelea vizuri na mazoezi, ushindani unaoonekana unaonyesha kila mmoja ana kiu ya kupata matokeo chanya katika mchezo huo.

Hafidh alisema wamejipanga kuhakikisha wanaendelea kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo kwa sababu wanahitaji kuibuka mabingwa wa msimu huu.

"Tumejipanga na kujiimarisha, tumerekebisha upungufu uliyokuwapo kwa ajili ya kurejea na kasi mpya, tunajua mechi zote ni ngumu, hivyo hatutabweteka," meneja huyo alisema.

Naye Ofisa Uhusiano wa KMC, Christina Mwangala, alisema timu yake itaingia uwanjani ikiwa na lengo la kusaka ushindi ili kujiimarisha katika msimamo na hatimaye kutimiza malengo waliyonayo.

Mwangala alisema wamejiandaa kukabiliana na ushindani kwa sababu kila timu imedhamiria kuondoka na alama tatu muhimu katika mchezo huo huku KMC inaamini hakuna kitakachoshindikana.

"Tunakwenda kwenye mchezo ambao kimsingi hautakuwa mwepesi kutokana na aina ya timu ambayo tunakutana nayo, ni nzuri, wanafanya vizuri, lakini pia wanaongoza ligi, hivyo mchezo utakuwa mgumu, pamoja na yote bado KMC FC tunasema kwamba tunakwenda kupambanania alama tatu na tunaimani kubwa ya kufanya vizuri katika mchezo wetu," alisema Mwangala.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza wenyeji KMC walifungwa mabao 2-1, goli pekee la kikosi hicho cha Manispaa ya Kinondi lilifungwa na Hassan Kabunda dakika ya 23.

# Simba, Al Ahly kazi iendelee

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Yatamba iko tayari kukamilisha kibarua kilichowapeleka na kuweka rekodi...

VIGOGO wa Afrika, Al Ahly, wanatarajiwa kuwakaribisha vinara wa Kundi A, Simba ya Tanzania, katika mechi ya kukamilisha hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Al Salam jijini Cairo nchini Misri, huku timu zote mbili zikiwa zimeshatinga hatua inayofuata.

Matokeo yoyote ya mechi ya leo itakayochezwa kuanzia saa 4:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki hayatabadilisha msimamo wa kundi hilo ambalo Simba inaongoza ikiwa na pointi 13, Al Ahly ikiwa ya pili na pointi nane mkononi, AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wakiwa na pointi nne na Al Merreikh ya Sudan yenye pointi mbili ikiburuza mkia.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa Februari 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, Wekundu wa Msimbazi walipata ushindi wa bao 1-0, shukrani kwa winga, Luis Miquessone aliyefunga.

**Itakuwa ni mechi ya wababe, kwa sababu Al Ahly itahitaji kuona inalinda heshima kwa kutofungwa mara mbili na klabu hiyo kutoka Tanzania.**

Wachambuzi wa masuala ya soka wanasema huenda mechi ya leo haitakuwa na mvuto kwa sababu hiyo na inawezekana timu zote zikachezesha baadhi ya wachezaji ambao si tegemeo na hawajawahi kuonekana katika mechi zilizopita ili kuwapumzisha baadhi yao kwa ajili ya mechi za robo fainali.

Hata hivyo, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema kwa mujibu wa Kocha Mkuu, Didier Gomes da Rosa, mabadiliko katika kikosi hicho yatakuwa machache sana.

"Tuko tayari kwa mechi, itakuwa nzuri sana kutokana na timu zote jinsi zilivyo kwa sasa na nimeongea na mwalimu, kaniambia kikosi kitakuwa na mabadiliko machache sana, lakini hakitatofautiana na kile kilichocheza na AS Vita hapa nyumbani Tanzania," alisema Manara.

Kiongozi huyo alisema pamoja na timu hiyo kuwa tayari imefuzu, lakini inataka pia kuweka rekodi ya kushinda ugenini, hasa kwenye ardhi ya Misri ndiyo maana imesafiri na kikosi kilichokamilika.

"Unakumbuka kilichotokea mwaka 2019. Tulifungwa mabao 5-0, hatutaki safari hii hicho kitu kitokee ndiyo maana unaona hata mechi hii pia tunaichukulia kwa uzito mkubwa," Manara alisema.

Alisema kwa sasa Simba ina uwezo huo na ina faida ya kufundishwa na kocha ambaye ana uzoefu na timu za nchi za Afrika Kaskazini, ikiwamo nchini Misri, hivyo anawajua vyema wapinzani wao.

"Hata umoja, umeongezeka kwenye timu, kuanzia wachezaji, benchi la ufundi, viongozi, wanachama na mashabiki. Wote sasa tunaongea lugha moja, na hii ndiyo asili ya mafanikio ya Simba," alisema Manara.

Aliongeza kikosi chao kimekwenda Misri kwa kazi moja ya kupambana na wote wako tayari kukamilisha jukumu hilo walilolifuata.

Mechi nyingine ya kundi hilo itakwenda Mjini Lubumbashi kati ya wenyeji AS Vita dhidi ya Al Merreikh, ambao nao wanacheza mchezo wa kukamilisha ratiba kwa sababu wameshaaga mashindano hayo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >